



SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR

**HOTUBA YA WAZIRI WA AFYA, USTAWI WA JAMII,
WAZEE, JINSIA NA WATOTO
MHESHIMIWA NASSOR AHMED MAZRUI**

**KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI
KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 KATIKA
BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR**

Mei, 2021

YALIYOMO

<i>Mada</i>	<i>Ukurasa</i>
MCHANGANUO WA VIFUPISHO	iii
UTANGULIZI.....	1
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA KIFEDHA KWA MWAKA 2020/2021	5
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MALENGO KWA MWAKA 2020/2021	8
PROGRAMU YA KINGA NA ELIMU YA AFYA	9
Huduma za UKIMWI, Kifua Kikuu, Ukoma na Homa ya Ini.....	10
Huduma za Kumaliza Malaria Zanzibar	12
Huduma Shirikishi za Afya ya Uzazi na Mtoto	14
Huduma za Uratibu wa Shughuli za Kinga na Udhibiti wa Maradhi ya Miripuko na ufuatiliaji wa maradhi	15
Huduma za Maradhi yasiyoambukiza.....	16
Huduma za Maradhi Yasiyopewa Kipaumbele	17
Huduma za Lishe	18
Huduma za Msingi za Matibabu ya Macho	18
Huduma ya Utoaji wa Elimu ya Afya.....	19
Huduma za Afya ya Mazingira	19
Huduma za Afya Bandarini	21
Huduma za Afya ya Wafanyakazi.....	22
Huduma za Afya ya Msingi ya Akili	23
PROGRAMU YA TIBA	24
Programu Ndogo Huduma za Matibabu.....	25
Huduma za Damu Salama.....	25
Huduma za Mabaraza ya Kitaaluma	25
Huduma za Vituo vya Mkono kwa Mkono	26
Huduma ya Upatikanaji, Uhifadhi na Usambazaji wa Dawa na Vifaa vya utibabu	27
Huduma za Tiba Asili na Tiba Mbadala.....	28
Programu Ndogo Huduma za Uchunguzi	29
Huduma za Chakula, Dawa na Vipodozi	29
Huduma za Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali	30
PROGRAMU YA HIFADHI YA JAMII, MAENDELEO YA JINSIA NA WATOTO	32
Programu Ndogo ya Hifadhi ya Jamii.....	32
Programu Ndogo ya Maendeleo ya Jinsia na Watoto	34

<i>Mada</i>	<i>Ukurasa</i>
PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA.....	38
Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji.....	38
Programu ndogo Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara	40
Taasisi ya Utafiti wa Afya Zanzibar	42
Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Afya Pemba.....	43
PROGRAMU YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA (H02).....	45
Programu ya Uchunguzi na Matibabu	45
Programu ndogo ya Uongozi wa Hospitali na Utawala	47
UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO	48
Ujenzi wa Maabara ya Uchunguzi ya Chakula, Dawa na Vipodozi	48
Ujenzi wa Bohari ya Dawa Pemba	48
Ujenzi wa Hospitali ya Wagonjwa wa Akili	48
Ujenzi wa Maabara ya Uchunguzi wa Virusi - Binguni	49
Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa na Kufundishia - Binguni	49
Ujenzi wa Wodi za Mama na Mtoto katika Hospitali ya Kivunge na Chake Chake	49
Ukarabati mkubwa wa Hospitali ya Wete na Ujenzi wa Nyumba za Wafanyakazi katika Hospitali ya Mkao ya Abdulla Mzee	50
CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA WAKATI WA UTEKELEZAJI.....	51
MWELEKEO WA BAJETI NA VIPAUMBELE VYA WIZARA, 2021/2022	52
SHUGHULI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2021/2022	54
PROGRAMU YA KINGA NA ELIMU YA AFYA (PH0301)	54
PROGRAMU YA TIBA (PH0302)	56
PROGRAMU HIFADHI YA JAMII, MAENDELEO YA JINSIA NA WATOTO (PH0303)	57
PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA (PH0305)	58
PROGRAMU YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA (H02).....	59
SHUKRANI.....	60
HITIMISHO	62
MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022	63

MAELEZO YA VIFUPISHO

- AMREF - Arica Medical Research Foundation
- BADEA - Arab Bank for Economic Development in Africa
- CCM - Chama cha Mapinduzi
- CDC - Center for Disease Control and Prevention
- COSTECH - Tanzania Commission for Science and Technology
- CUHAS - Catholic University of Health and Allied Sciences
- DNA - Deoxyribonucleic Acid
- EAC - East African Community
- ECHO - Echocardiography
- e-IDSR - electronic Integrated Disease Surveillance and Response
- e-LMIS - electronic Logistic Management Information System
- GFATM - Global Fund to Fight AIDS, Tuberculosis and Malaria
- HSSP IV - Health Sector Strategic Plan IV
- IHI - Ifakara Health Institute
- IHR - International Health Regulations
- IOM - International Organization of Migration
- JHPIEGO - Johns Hopkins Program for International Education in Gynecology and Obstetrics
- KCMUCO - Kilimanjaro Christian Medical University College
- MOU - Memorandum of Understanding
- MRI - Magnetic Resonance Imaging

MUHAS	- Muhimbili University of Health and Allied Sciences
NIMR	- National Institute for Medical Research
PEPFAR	- President's Emergency Plan for AIDS Relief
PHCU+	- Primary Health Care Unit +
PMI	- President's Malaria Initiatives
RCH	- Reproductive and Child Health
SUZA	- State University of Zanzibar
TB	- Tuberculosis
TV	- Television
UAE	- United Arab Emirates
UDOM	- University of Dodoma
UNDP	- United Nations Development Program
UNFPA	- United Nations Population Fund
UNICEF	- United Nations International Children Emergency Fund
USAID	- United States Agency for International Development
VVU	- Virusi Vya UKIMWI
WHO	- World Health Organization
ZALIRI	- Zanzibar Livestock Research Institute
ZAWA	- Zanzibar Water Authority
ZBS	- Zanzibar Bureau of Standard
ZFDA	- Zanzibar Food and Drug Agency

UTANGULIZI

- 1. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja Baraza lako likae kama Kamati ya Matumizi kwa ajili ya kupokea, kujadili na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kwa mwaka wa fedha 2021/2022.
- 2. Mheshimiwa Spika**, kwanza kabisa naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma aliyeumba mbingu na ardhi na vyote viliomo baina yake, kwa kutujaalia uhai, uzima na afya njema; hali iliyopelekea kukutana katika kikao hiki cha kwanza cha kujadili bajeti tokea kuanza kwa shughuli za Baraza la 10 la Wawakilishi, Zanzibar. Aidha, natoa shukrani za pekee kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi **Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi** kwa kupata ushindi katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2020, ambao umemuwezesha kuwa Rais wa Serikali ya Awamu ya Nane (8). Ni dhahiri kwamba katika uongozi wake ameonesha umahiri wa kuiongoza nchi hii ndani ya kipindi kifupi baada ya kuingia madarakani. Pia, niwapongeze **Mheshimiwa Othman Masoud Othman** Makamo wa Kwanza wa Rais na **Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdullah** Makamo wa Pili wa Rais kwa uteuzi waliouopata wa kuwa wasaidizi wakuu wa Mheshimiwa Rais.

3. **Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya kipekee nachukuwa fursa hii kumpongeza **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan** kwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na pia kuwa mwanamke wa kwanza kushika wadhifa huo katika historia ya nchi yetu. Ni ukweli usiopingika kwamba amekuwa kiongozi wa mfano katika kuliongoza Taifa hili; hekma, busara na ujasiri alionao umedhihirisha kwa vitendo kwamba “**Wanawake Wanaweza**”. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ampe afya njema, nguvu, maarifa pamoja na maamuzi yenyе kuleta tija kwa maendeleo ya Watanzania.
4. **Mheshimiwa Spika**, naomba pia nikupongeze wewe binafsi kwa kuendelea kuwa Spika wa Baraza la Wawakilishi pamoja naibu wako **Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma**; kitendo cha ukomavu na umahiri mkubwa mliouonesha katika kuendesha na kusimamia chombo hiki ni sababu tosha kwa Wajumbe wa Baraza hili kuwapa ridhaa ya kuendelea na jukumu hili kwa kipindi chengine. Aidha, niwapongeze Wenyeviti wawili pamoja na wajumbe wote mlio chaguliwa kuingia katika Baraza hili. Ni imani ya wananchi waliowachagua kwamba mtawatendea haki ya kuwawakilisha katika chombo hiki cha kuitisha masuala yote yenyе mustakbali wa nchi hii.
5. **Mheshimiwa Spika**, sote tunatambua kwamba mwaka 2021 nchi yetu ilikumbwa na misiba mizito, ambayo itaendelea kuwepo katika nyoyo za Watanzania; kwa niaba ya Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto hatuna budi kutoa pole kwa

Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, viongozi na wanachama wa ACT- Wazalendo pamoja na Wazanzibari wote kwa kumpoteza Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar Almarhum **Maalim Seif Sharif Hamad**, ambaye pia alikuwa ni mshauri wa karibu wa Mheshimiwa Rais. Kifo chake kimetokea wakati ambao nchi yetu inaelekea katika mageuzi ya kuondosha imani tofauti na mifarakano miongoni mwa jamii, hakika msiba huu umewagusa Wazanzibari na Watanzania wote kwa ujumla. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aihifadhi roho yake katika bustani za waja wema peponi Amin.

6. **Mheshimiwa Spika**, tukio jengine ambalo Watanzania hawatolisahau ni lile la kuondokewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Tano (5) Hayati **Dkt. John Pombe Magufuli** pamoja na kifo cha **Mzee Benjamin William Mkapa**; viongozi hawa wamekuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya histroria nchi yetu. Watanzania tutaendelea kuwaenzi na kuendeleza yale mazuri waliyotuachia. Hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa nchi yetu kuendelea kuwa na amani na utulivu mkubwa licha ya matukio haya yaliyotokea. Aidha, nichukuwe fursa hii pia, kuwapa pole wanachama wa ACT Wazalendo, familia na wananchi wa Jimbo la Pandani kutokana na kifo cha aliyekuwa Mwakilishi mteule wa Jimbo hilo **Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakari**, Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi, Amin.

7. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa Wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii inayoongozwa na **Mheshimiwa Yahya Rashid Abdallah**, hivyo nachukuwa fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa namna walivyoshirikiana nasi wakati wote walipofanya ziara katika Wizara hii. Wameonesha uweledi na ukomavu mkubwa katika kutupatia maelekezo, ushauri na mapendekezo ya kuimarisha utendaji kwa nia ile ile ya kufikia malengo ya Serikali ya Awamu ya nane (8). Aidha, Wizara inawashukuru sana kwa kuyapitia mapendekezo ya bajeti ya mwaka 2021/2022 na kutupatia michango mingi, ambayo imeweza kuandaa hotuba hii ninayoisoma mbele ya baraza lako.
8. **Mheshimiwa Spika**, itakumbukwa kwamba katika hotuba ya bajeti ya mwaka 2020/2021, Wizara ya Afya iliwaeleza wananchi kuititia Baraza hili kuibuka kwa ugonjwa wa Korona hapa Zanzibar; ugonjwa uliosababisha vifo na madhara makubwa kwa wananchi wetu. Napenda kuchukuwa fursa hii kuwashukuru wananchi wote. kwa usikivu wao wa kufuata masharti waliyopewa na wahudumu wa afya, jambo ambalo limefanikisha kupunguza kwa kiasi kikubwa maradhi ya Korona. Katika kipindi hiki cha utekelezaji wa bajeti kumeibuka ugonjwa mwengine wa shida ya kupumua uliozikumba familia nyingi, ambao nao umepungua sana. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ailinde nchi yetu na majanga ya maradhi ya namna hii yasitokee tena. Aidha, Wizara inawaomba wananchi waendelee kuchukua hatua za tahadhari kadri zinavyotolewa na wataalamu wa afya.

9. **Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo sasa naomba uniruhusu kutoa taarifa ya utekelezaji wa Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kama ifuatavyo:-

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA KIFEDHA KWA MWAKA 2020/2021

10. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara ya Afya Fungu H01 (kabla kuunganishwa) ilikadiriwa kutumia shilingi **100,236,100,000** zikiwemo shilingi **19,351,500,000** kwa ajili ya mishahara; shilingi **35,313,100,000** kwa kazi za uendeshaji wa ofisi; shilingi **2,924,400,000** zilipangwa kwa taasisi zinazopata ruzuku na shilingi **42,647,100,000** kwa kazi za miradi ya maendeleo. Aidha, kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Wizara ilipangiwa kutumia shilingi **31,177,445,197** kwa shughuli za uendeshaji; shilingi **14,513,625,000** kwa ajili ya mishahara na maposho; shilingi **2,193,300,001** zilitengwa kwa taasisi zinazopata ruzuku na shilingi **37,052,661,772** kwa kazi za miradi ya maendeleo.
11. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi 2021, Wizara ya Afya (H01) iliingiziwa jumla ya shilingi **15,409,550,831** sawa na asilimia **49.4** ya fedha zilizotengwa katika kipindi hicho kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji; shilingi **16,630,564,687** zaidi ya asilimia mia ziliingizwa kwa ajili ya mishahara; shilingi **1,550,346,464** (asilimia 70.7) zilitolewa kwa taasisi zinazopata ruzuku; na shilingi **5,566,760,907** (asilimia 15.0) kwa shughuli za miradi ya maendeleo.

- 12. Mheshimiwa Spika**, programu ya Hifadhi ya Jamii na Maendeleo ya Wanawake na Watoto ilitengewa shilingi **11,553,794,096**; kati ya hizo shilingi **10,544,035,080** kwa shughuli za ustawi wa jamii na shilingi **1,009,759,016** kwa ajili ya huduma za wanawake na watoto. Kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, programu ndogo ya ustawi Jamii ilipangiwa kutumia shilingi **7,908,026,310** na programu ndogo ya maendeleo ya wanawake na watoto walipangiwa matumizi ya shilingi **757,319,262**. Hadi kufikia Machi, 2021 programu ndogo ya ustawi wa jamii iliingiziwa shilingi **6,236,774,070** sawa na asilimia 78.9 na maendeleo ya wanawake na watoto wameingiziwa shilingi **176,056,685** (asilimia 23.2).
- 13. Mheshimiwa Spika**, Hospitali ya Mnazi Mmoja (Fungu H02) imekadiriwa kutumia shilingi **17,348,600,000**; matumizi ya shilingi **12,249,400,000** yalipangwa kwa ajili ya mishahara na shilingi **5,099,200,000** kwa kazi za uendeshaji wa hospitali. Kwa kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021; Hospitali hiyo ilitengewa kutumia shilingi **13,820,582,919**; kati ya hizo shilingi **4,633,532,922** kwa shughuli za uendeshaji na shilingi **9,187,049,997** kwa ajili ya mishahara na maposh. Hadi kufikia Machi, 2021 jumla ya shilingi **2,581,051,896** sawa na asilimia **55.7** ziliingizwa kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji na shilingi **10,057,978,258** (asilimia 109.5) kwa malipo ya mishahara na maposh. Kwa ujumla asilimia ya fedha zilizopatikana kwa mwaka wa fedha 2020/2021 inaonekana katika **Kiambatisho namba 1**.

- 14. Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Afya ilitakiwa kukusanya shilingi **360,505,000** na Hospitali ya Mnazi Mmoja ilipangia kukusanya shilingi **675,000,000** kutoka katika vyanzo vya mapato kwa ajili ya kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali. Hadi kufikia Machi 2021, jumla ya shilingi **1,634,037,018** zilikusanywa kutoka katika vyanzo vya Wizara (H01) na shilingi **580,793,374** zilikusanywa na Hospitali ya Mnazi Mmoja. Fedha zote zilizokusanywa ziliingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali. **Kiambatisho namba 2** kinafafanua fedha zilizokusanywa kwa mujibu wa vyanzo vya mapato.
- 15. Mheshimiwa Spika**, fedha hizo zilizotengwa zililenga kufanikisha malengo yaliyowekwa na Wizara kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021. Miongoni mwa malengo hayo ni: -
- i. Kuweka mfumo endelevu wa fedha kwa kugharamia huduma za afya;
 - ii. Kuendelea na ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya kisasa na Kufundishia ya Binguni;
 - iii. Kufanya ukarabati wa Hospitali za Wilaya na Mkoa;
 - iv. Kukamilisha ujenzi wa Maabara ya Utafiti wa uchunguzi wa maradhi yanayosababishwa na virusi (Virology);
 - v. Kuanzisha Idara ya Uchunguzi wa Maabara; na
 - vi. Kuanzisha huduma za matibabu ya upasuaji wa moyo.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MALENGO KWA MWAKA 2020/2021

16. Mheshimiwa Spika, shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2020/2021 zilizingatia mikakati ya kitaifa na kimataifa, sera mbali mbali pamoja na llani za Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi -CCM (2015-2020). Katika kipindi cha utekelezaji, Wizara imepata mafanikio mengi kupitia shughuli zilizofanywa na idara na vitengo vilivyopo kwa ajili ya kufikia malengo yaliyokusudiwa kwa mujibu wa shabaha zilizowekwa. Baadhi ya mafanikio makubwa yaliyopatikana ni pamoja na: -

- i. Kukamilika kwa jengo la ghorofa mbili la huduma za mama na mtoto katika Hospitali ya Wilaya ya Kivunge;
- ii. Kufikia hatua za mwisho za ujenzi wa jengo la Hospitali ya Wagonjwa wa Akili Kidongo Chekundu;
- iii. Kukamilika kwa ujenzi wa Bohari ya Dawa Pemba;
- iv. Kuongezeka kwa idadi ya madaktari bingwa;
- v. Kuzinduliwa kwa Mkakati wa Miaka 5 wa Dijitali wa Afya (Digital Health Strategy);
- vi. Kukamilika kwa Mpango Mkakati wa Ubora wa Huduma na Mpango Mkakati wa Taarifa za Afya; na
- vii. Kuanzisha uchunguzi wa maradhi ya mripuko ikiwemo Korona katika Maabara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja.

17. Mheshimiwa Spika, naomba kuyaelezea kwa kina mafanikio hayo katika utekelezaji wa shughuli zilizofanyika kupitia huduma zinazotolewa katika kila programu husika kama ifuatavyo:-

PROGRAMU YA KINGA NA ELIMU YA AFYA

- 18. Mheshimiwa Spika**, sote tunaelewa kwamba kinga ni bora kuliko tiba. Hivyo, jukumu kuu la programu hii ni kuhakikisha jamii inapata huduma bora za kinga pamoja na kuongeza uelewa juu ya njia za kujikinga na maradhi mbali mbali ya kuambukiza na yasiyoambukiza yakiwemo maradhi ya miripuko. Wizara ilitenga jumla ya shilingi **28,664,931,000**; ambapo hadi kufikia Machi, 2021 shilingi **5,431,942,196** sawa na asilimia **18.9** ziliingizwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli zilizopangwa katika programu hii zikiwemo:-
- i. Kuandaa Mpango Mkakati wa Maradhi yasiyoambukiza;
 - ii. Kuhakikisha Sera ya Udhibiti wa tumbaku inafanyiwa kazi kikamilifu kuanzia ngazi ya taifa hadi jamii;
 - iii. Kuendelea kufanya shughuli za ufuatiliaji wa mienendo ya maradhi;
 - iv. Kuandaa muongozo wa maradhi yasiopewa kipaumbele;
 - v. Kufanya utafiti wa kujua kiwango cha minyoo katika jamii;
 - vi. Kuendelea kutekeleza mpango wa Kumaliza Malaria Zanzibar; na
 - vii. Kutekeleza Muongozo wa Kimataifa wa Afya (International Health Regulation -IHR) katika kudhibiti maradhi ya kuambukiza.
- 19. Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa shughuli hizi umefanyika kupitia huduma zilizotolewa katika vitengo vya programu hii kama ifuatavyo:-

Huduma za UKIMWI, Kifua Kikuu, Ukoma na Homa ya Ini

- 20. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha utekelezaji jumla ya watu **181,322** (wanawake - 103,318 na wanaume - 7,804) walichunguzwa VVU. Kati yao watu **1,279** (wanawake - 839 na wanaume - 440) sawa na asilimia **0.7** ya waliochunguzwa wamegundulika na VVU. Hadi sasa, jumla ya watu **7,185** (wanaume 2,241 na wanawake 4,944) wanaoishi na VVU wanaendelea kupatiwa huduma na tiba kwenye kliniki **14** (Unguja 10 na Pemba 4) zinavyotoa huduma hizi. Miongoni mwa watu hao; **7,111** (wanawake - 4,893 na wanaume - 2,218) sawa na asilimia **99** ya waathirika wanatumia dawa za kupunguza makali ya VVU (ARVs).
- 21. Mheshimiwa Spika**, wajawazito **46,050** waliohudhuria kliniki walipatiwa huduma ya upimaji wa VVU, wajawazito **71** (asilimia 0.2) waligunduliwa na maambukizo; ambapo wajawazito **66** walipewa dawa za ARVs. Aidha, watoto **213** waliozaliwa na mama walioathirika na VVU walichunguzwa kwa kipimo cha DNA-PCR, ambapo watoto watatu (**3**) wameonekana na maambukizi ya VVU na wanaendelea kupatiwa matibabu.
- 22. Mheshimiwa Spika**, zoezi la ufuatiliaji wa wagonjwa wa VVU waliopo katika matibabu lilifanyika; jumla ya sampuli za damu **1,238** zimekusanywa na kuangaliwa kiwango cha VVU katika Hospitali za Mnazi Mmoja, Kivunge na Chake Chake. Kati ya

sampuli zilizochunguzwa, sampuli **1,162** sawa na asilimia **93.9** zimeonekana kuwa na kiwango cha chini ya kopi **1,000** za virusi na kufikia lengo la kimataifa la asilimia **90** ya kufubaza kiwango cha virusi (Viral Load Supression).

23. **Mheshimiwa Spika**, jumla ya watu **30, 958** walichunguzwa virusi ya homa ya Ini B na C; (wanawake – 11,368 na wanaume -19,550) kuititia huduma mbali mbali zinazotolewa katika hospitali na vituo vya afya, zikiwemo huduma za kliniki za mama na mtoto na huduma za uchangiaji damu kwa Unguja na Pemba. Watu **370** (wanawake - 180 na wanaume - 190) sawa na asilimia 1.6 ya watu **25,923** waliochunguzwa virusi ya homa ya Ini B wamegundulika na maambukizo (Unguja – 292 na Pemba – 58). Aidha, watu **49** (wanawake - 3 na wanaume - 46) sawa na asilimia 1.2 ya watu 5,035 ya waliochunguzwa homa ya Ini C wamegundulika na maambukizo (wote kutoka Unguja). Kwa sasa, jumla ya wagonjwa **1,497** wanaendelea na matibabu; Mnazi Mmoja (1,309), Hospitali ya Kivunge (13) na Hospitali ya Chake Chake (175). Jumla ya watu **88** wenye maambukizo ya virusi vya homa ya Ini **B** wanatumia dawa za ARVs.
24. **Mheshimiwa Spika**, jumla ya watu **86** wapya (wanawake - 2 na wanaume - 84) wanaotumia dawa za kulevya wamesajiliwa kwenye kituo kinachotoa huduma ya “Methadone” katika Hospitali ya Kidongo Chekundu Unguja, ambapo wateja **wanane** (8); wanaume **sita** (6) na wanawake **wawili** (2) walipona na kuruhusiwa. Kiujumla wateja **869** (wanawake - **43** na wanaume - **826**) wanaendelea na matibabu.

- 25. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hiki cha utekelezaji, jumla ya wagonjwa wa ukoma **84** (Unguja 73 na Pemba 11) wamegundulika, mionganini mwao wagonjwa **25** sawa na asilimia **73** waligundulika na ukoma wenyewe mabaka mengi ambao unaambukiza katika jamii na wagonjwa watano (5) sawa na asilimia **26.4** ni wenyewe mabaka kidogo ambao hawaambukizi. Aidha, wagonjwa **16** sawa na asilimia **48** ya wagonjwa hao waligundulika kuwa na ulemavu wa daraja la awali, wagonjwa **13** waligundulika kuwa na ulemavu wa kati na wagonjwa **5** kuwa na ulemavu wa daraja la juu. Katika kupambana na kifua kikuu, jumla ya wagonjwa wapya **801 (525)** Unguja na **276** Pemba) waligundulika na kifua kikuu na kuanzishiwa matibabu katika kipindi hiki.

Huduma za Kumaliza Malaria Zanzibar

- 26. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021 jumla ya wagonjwa **1,630,320** (Unguja - 1,136,463 na Pemba - 493,857) walihudhuria katika hospitali na vituo vya afya; kati yao, wagonjwa **440,715** (Unguja - 379,892 na Pemba - 60,823) walichunguzwa vimelea vya malaria, ambapo wagonjwa **6,626** (Unguja - 6,090 na Pemba - 536) sawa na asilimia **1.5** waligunduliwa kuwa na vimelea vya ugonjwa huo na kupatiwa tiba stahiki. Wagonjwa **6,129** sawa na asilimia **92.5** ya walibainika kuwa na vimelea vya malaria walifuatiliwa majumbani kwa lengo la kuangalia chanzo cha maambukizo hayo.
- 27. Mheshimiwa Spika**, maeneo yaliyori potiwa kuwa na wagonjwa wengi wenyewe vimelea vya malaria ni kutoka Wilaya za Mjini, Magharibi B na Magharibi A. Idadi kubwa ya wagonjwa

imechangiwa na mabadiliko ya hali ya hewa yaliyosababisha na kuwepo kwa mvua kubwa. Aidha, katika kuongeza ufanisi wa ugunduzi wa vimelea vya malaria, wizara imenunua kipimo cha haraka chenye uwezo wa kugundua kiwango kidogo kabisa cha vimelea vya malaria katika damu.

- 28. Mheshimiwa Spika**, zoezi la ufuatiliaji na uhakiki wa vimelea vya malaria kwa njia ya hadubini lilifanyika katika vituo vya afya **98** Unguja na Pemba, ambapo matokeo yameonyesha kwamba asilimia 81.5 ya vimelea ni vya aina ya *Plasmodium falciparum*. Mazalia **38** (Unguja 30 na Pemba 8) yenye viluilui vya mbu wa malaria yaliyogundulikana katika shehia **14** zenye madimbwi yenye mazalia ya mbu yamewekewa dawa ya kuulia vimelea.
- 29. Mheshimiwa Spika**, zoezi la upigaji dawa majumbani lilifanyika katika shehia 67 (Unguja- **56** na Pemba -**11**), ambapo jumla ya nyumba **46,315** (Unguja - 37,526 na Pemba - 8,789) katika Shehia zilizomo katika Wilaya hizo zilipigwa dawa. Zoezi hilo lilifanikiwa kwa zaidi ya asilimia 100 (makadirio nyumba 45,965). Katika muendelezo huo huo wa kumaliza malaria Zanzibar, jumla vya vyandarua **415,217** (Unguja 314,108 na Pemba 101,009) viligawiwa kwa wanajamii kuitia vituo vya afya vinavyotoa huduma za ugawaji wa vyandarua Unguja na Pemba. Aidha, vyandarua **197,000** viligaiwa katika Mkoa wa Mjini Magharibi kutokana na kuibuka kwa ongezeko la ugonjwa wa malaria na upungufu wa vyandarua katika jamii.

Huduma Shirikishi za Afya ya Uzazi na Mtoto

- 30. Mheshimiwa Spika**, wizara inaendelea kuchukuwa juhudzi mbali mbali katika kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi. Miongoni mwa juhudzi hizo ni kufanya uhakiki wa vifo hivyo ili kubaini sababu zilizopelekea kutokea kwake na kuchukua hatua stahiki. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi, 2021, vifo vya mama **44** na watoto wachanga **1,201** viliripotiwa katika hospitali zinazotoa huduma za uzazi. Vifo vya mama **28** (asilimia 63) na vya watoto wachanga **446** (asilimia 37) vilihakikiwa. Matokeo ya uhakiki huo yamebainisha sababu za vifo hivyo ni pamoja na watoto kukosa hewa wakati wa kuzaliwa; uzito pungufu; njiti; kupoteza damu na maambukizi kwa watoto wachanga. Kwa upande wa vifo vya mama ni kifafa cha mimba, upungufu wa damu wakati wa ujauzito, kupoteza damu wakati wa ujauzito pamoja na kisukari na maradhi mengine sugu wakati wa ujauzito.
- 31. Mheshimiwa Spika**, juhudzi za kuwashajihisha akina mama kuhudhuria kliniki ya wajawazito pamoja na kujifungulia katika hospitali na vituo vya afya zimeendelea kuchukuliwa na kuonesha mafanikio. Jumla ya mama wajawazito **46,050** walihudhuria kliniki ya upimaji mimba angalau mara moja katika kipindi cha ujauzito. Idadi hii ni kubwa ukilinganisha na wajawazito **40,177** kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Aidha, katika kipindi hicho, wajawazito **33,057** (asilimia 61.3) walijifungua katika hospitali za Unguja (22,164) na Pemba (10,893).

32. Mheshimiwa Spika, kama nilivyoleza mwanzoni mwa program hii kwamba moja ya lengo la wizara ni kuikinga jamii dhidi ya maradhi ambayo yanaweza kuepukika. Kwa mustakbali huo, Wizara imeendelea kutoa chanjo kwa watoto chini ya umri wa mwaka mmoja ambapo watoto **36,288** sawa na asilimia **89.5** ya walengwa walipatiwa chanjo ya Penta 3 na wasichana **7,361** wenye umri wa miaka 14 walipatiwa chanjo ya saratani ya mlango wa kizazi.

Huduma za Uratibu wa Shughuli za Kinga na Udhiliti wa Maradhi ya Miripuko na ufuatiliaji wa maradhi

33. Mheshimiwa Spika, shughuli za kuratibu kinga ya maradhi ya miripuko na majanga ya kiafya ziliendelea kufanyika sambamba na utoaji wa huduma za upimaji wa virusi vya Korona kwa wasafiri wa nje ya nchi. Tokea kuanza kwa maabara ya kupimia virusi vya Korona hapa Zanzibar (Oktoba 2020), jumla ya wasafiri **39,523** (wageni 31,794 na wenyeji 7,729) wamefanyiwa vipimo. Jumla ya vituo **vitano** (5) vinatumika kuchukulia vipimo vya Korona; vituo hivyo ni Lumumba, Migombani, Makunduchi na Hospitali ya Global kwa Unguja na Mfikiwa kwa upande wa Pemba. Kwa ujumla kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya wasafiri **53,796** (wageni 45,224 na wenyeji 8,572) wameripotiwa kufanyiwa vipimo vya Korona. Kuanzia mwezi Machi 2021, huduma za usajili, malipo na utoaji wa vyeti unafanyika kielektroniki, jambo ambalo limeongeza ufanisi, kupunguza usumbufo kwa wasafiri na utolewaji wa vyeti bandia.

- 34. Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO) imefanya tathmini ya mpango wa kukabiliana na ugonjwa wa Korona. Lengo la tathmini hii ni kuangalia mafanikio na changamoto katika kukabiliana na ugonjwa huo. Aidha, muongozo mpya wa ufuutiliaji wa mienendo ya maradhi ulifanyiwa mapitio ili uendane na mazingira halisi ya Zanzibar. Jumla ya maofisa ufuutiliaji wa maradhi **20** (Unguja - 14 na Pemba - 6) walipatiwa mafunzo ya ufuutiliaji wa magonjwa pamoja na matukio ya kiafya kwa kutumia mwongozo huu.
- 35. Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa mpango wa kutokomeza Kipindupindu Zanzibar, Wizara imenunua mahema **10** (Unguja -7 na Pemba - 3). Mahema hayo yatatumika katika vituo vya kutoa matibabu ya maradhi ya kipindupindu. Aidha, pikipiki 11 zimepelekwa katika Wilaya za Unguja na Pemba kwa ajili ya ufuutiliaji wa kazi za mpango wa kutokomeza Kipindupindu Zanzibar.

Huduma za Maradhi Yasiyoambukiza

- 36. Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea kuimarisha uchunguzi na matibabu ya maradhi yasiyoambukiza kupitia hospitali, vituo vya afya na ngazi ya jamii. Juhudi zaidi zimeelekezwa katika kuongeza uelewa katika ngazi ya jamii juu ya maradhi haya na vichocheo vyake. Jumla ya wanawake **569** wamechunguzwa saratani ya matiti kupitia kampeni maalum za jamii; kati yao, wanawake **105** wamegunduliwa na uvimbe wa matiti, **45** walipewa rufaa kwenda Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa ajili ya uchunguzi na **wanne** (4)

walifanyiwa upasuaji wa matiti. Aidha, Wizara inaendelea kusajili wagonjwa wa saratani na taarifa zao kwa ujumla katika rejista maalum la wagonjwa wa saratani, ambapo jumla ya wagonjwa **103** wameorodheshwa.

- 37. Mheshimiwa Spika**, katika hatua nyengine, watu **200** walifanyiwa uchunguzi wa maradhi mbali mbali yasiyoambukiza katika jamii, kati yao **21** walionekana katika hatari ya kupata kisukari; **watano** (5) waligundulika na kisukari; **10** walikuwa na uzito mdogo; **68** walikuwa na uzito uliokithiri; **97** waligundulika na hatari ya kupata shinikizo la damu na **saba** (7) wana tatizo la shinikizo la damu. Sambamba na zoezi hilo lililofanywa katika jamii, jumla ya wauguzi **274** walifanyiwa uchunguzi katika siku ya kisukari duniani. Katika uchunguzi huo, wauguzi **11** waligundulika na ugonjwa kisukari, wauguzi **20** walikutwa na shinikizo la damu, wauguzi **76** walikuwa na uzito mkubwa na **94** walikuwa na unene uliokithiri (obesity).

Huduma za Maradhi Yasiyopewa Kipaumbele

- 38. Mheshimiwa Spika**, Wizara imekamilisha kuandaa rasimu ya awali ya Mwongozo wa Udhhibit wa Maradhi Yasiyopewa Kipaumbele Zanzibar, mwongozo huo unategemewa kukamilika mwishoni mwa mwezi Julai 2021. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la SCORE pamoja na Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO) imefanya utafiti wa kuangalia kiwango cha Minyoo na Kichocho katika jamii. Jumla ya Shehia **94** zimefanyiwa utafiti huo Unguja na Pemba. Matokeo ya utafiti huu yanategemewa kutolewa baada ya kukamilika kwa uchambuzi na uhakiki wa takwimu.

- 39. Mheshimiwa Spika**, zoezi la ulishaji dawa za minyoo na matende lilifanyika katika skuli na majumbani; jumla ya watu **1,207,179** (Unguja 868,710 na Pemba – 338,469) wamepewa dawa za kinga ya maradhi hayo.

Huduma za Lishe

- 40. Mheshimiwa Spika**, Wizara ilifanya zoezi la ulishaji wa matone ya Vitamin A, dawa za minyoo na upimaji wa hali ya lishe. Jumla ya watoto **155,183** wenye umri wa miezi sita hadi miaka mitano walipatiwa matone ya Vitamin A, amba ni sawa na asilimia **66.7** ya watoto **232,748** waliotarajiwa. Aidha, watoto **110,571** wenye umri wa kuanzia mwaka mmoja hadi miaka mitatu walipatiwa dawa za minyoo.

Huduma za Msingi za Matibabu ya Macho

- 41. Mheshimiwa Spika**, uchunguzi wa macho katika jamii ulifanyika kwenye vijiji **10** vya shehia za Fumba, Bweleo, Matemwe, Kijini, Pwani Mchangani na Tazari. Wananchi **1,109** walichunguzwa, kati yao wananchi **700** walipatiwa matibabu ya papo hapo, wananchi **438** walipatiwa miwani ya kusomea na watu **409** walipewa rufaa ya kuendelea na matibabu katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Aidha, huduma hizo za uchunguzi pia zilifanyika wakati wa maonyesho ya biashara ya maadhisho ya miaka **57** ya Mapinduzi ya Zanzibar, Jimbo la Mwembe Makumbi na walimu wa Skuli ya Mwembeshauri. Jumla ya watu **1,001** (wanaume **455** na wanawake **546**) walibainika kuwa na matatizo ya macho yakiwemo uoni hafifu na mtoto wa jicho.

Huduma ya Utoaji wa Elimu ya Afya

42. Mheshimiwa Spika, elimu ya afya ni huduma ya msingi katika kuwezesha jamii kujikinga na maradhi mbali mbali. Katika kufanikisha azma hii, walimu **1,533** wa skuli za msingi Unguja na Pemba walipatiwa mafunzo juu ya maradhi ya miripuko. Pia, vipindi mbali mbali vya redio na TV vilirushwa hewani vikiwa na mada za jinsi ya kujikinga na Korona, Ebola, malaria, umuhimu wa kunawa mikono, matunzo ya watoto wakati wa Korona na madhara ya kijamii. Aidha, “posters” **44,000** na vipeperushi **32,000** vilisambazwa kwa ajili ya kuelimisha wananchi kuhusiana na unawaji sahihi wa mikono na njia nyengine za kujikinga na maradhi ya miripuko. Elimu ya afya kwa jamii imetolewa kupitia njia tofauti zikiwemo magari ya matangazo, maigizo ya Sanaa na usambazaji wa vipeperushi. Wahudumu wa afya wa kujitolea **1,100** wa Wilaya za Mjini na Magharibi “A” Unguja walipatiwa mafunzo ya msingi ya matumizi ya simu katika kukusanya na kutuma taarifa za afya katika mfumo wa ‘Jamii ni Afya’.

Huduma za Afya ya Mazingira

43. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa jamii inatumia maji safi na salama, Wizara imegawa dawa za kutibu maji ambapo vidonge **1,361,090** viligawiwa katika shehia **46** zilizobainika kuwa na shida kubwa zaidi ya upatikanaji wa maji kutoka Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA). Shehia hizo ni kutoka Wilaya ya Mjini (7), Magharibi ‘A’ (7) na Magharibi ‘B’ (11), Wete (11) na Micheweni (10). Jumla ya watu **224,598** walinufaika na zoezi hili.

- 44. Mheshimiwa Spika**, zoezi la ukaguzi katika vituo 10 vya mamlaka ya maji Zanzibar (ZAWA) vinavyohifadhi maji lilifanyika kwa lengo la kuangalia usalama wa maji kwa mtumiaji. Matokeo ya ukaguzi huo yamebainisha kwamba vituo vya Saateni, Dole, Chake Chake, Kaburikikombe na Mnarawambao vilikuwa na mfumo wa kutibu maji unaofanyakazi vizuri na vituo vya Mombasa, Welezo, Kinuni, Mtopepo na Wete havikuwa na mfumo wa kutibu maji. Kufuatia hali hiyo, taratibu za kutibu maji hayo zilichukuliwa. Katika hatua nyengine, ili kuhakikisha maji yanayotolewa katika taasisi na maeneo husika yanatibiwa, Wizara ilitoa mafunzo ya kutibu maji kwa walimu **21**, watoa huduma za kujitolea katika ngazi ya jamii **45** na maafisa **51** wa afya ya mazingira.
- 45. Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza Mpango wa Kutokomeza Kipindupindu Zanzibar, Wizara imefanya kampeni ya usafi wa afya na mazingira iliyojumuisha mashindano yalijotathmini hali ya usafi katika Halmashauri na Mabaraza ya mji yaliyomo katika wilaya za Mjini, Magharibi A, Magharibi B, Wete, Micheweni pamoja na vituo vya afya na skuli za msingi zilizomo katika maeneo hayo, ambayo yanapata zaidi miripuko ya kipindupindu. Mashindano haya yalitathmini udhibiti wa taka ngumu na za maji, matumizi ya maji safi na salama, utoaji wa huduma za afya zinazozingatia kudhibiti maambukizi wakati wa utoaji wa huduma. Matokeo ya tathmini hii yamebainisha kwamba hali ya usafi wa mazingira kwa Pemba ni asilimia **44** na asilimia **40.5** kwa Unguja, kiwango hiki kinaonesha kwamba bado miji yetu inahitaji kufanyiwa kazi katika suala la usafi wa mazingira.

- 46. Mheshimiwa Spika**, katika kudumisha hali ya usafi wa mazingira na kudhibiti kuenea kwa maambukizo katika vituo vya afya na jamii, Wizara imejenga vinu vya kuchomea taka katika hospitali (incinerators) **tano (5)** katika vituo vya Fuoni, Selem na Matemwe kwa Unguja na Hospitali ya Wete na Kituo cha Afya Kojani kwa Pemba. Pia, Wizara imefanya mafunzo kwa watumishi **74** wa afya juu ya kudhibiti maambukizo pamoja na kufanya marekebisho ya miundombinu ya upatikanaji wa maji na unawaji wa mikono katika vituo vya afya **13** vya Unguja.

Huduma za Afya Bandarini

- 47. Mheshimiwa Spika**, jumla ya wageni **462,222** waliingia nchini, kati yao wasafiri **299,805** walipitia bandarini na **162,417** walipitia uwanja wa ndege. Wasafiri hao walifanyiwa uchunguzi na ufuutiliaji, ambapo hakuna mgeni aliyeripotiwa kuwa na maradhi ya kuambukiza. Aidha, jumla ya maiti **68** na wagonjwa **148** walipitishwa na kukaguliwa Bandarini na uwanja wa ndege, ambapo wagonjwa **wanne (4)** walibainika na dalili za Korona na kupelekwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa hatua zaidi.
- 48. Mheshimiwa Spika**, jumla ya wasafiri wa nje ya nchi **824** walipatiwa chanjo za wasafiri ikiwemo chanjo ya homa ya manjano (**774**) na homa ya Ini B (**50**). Idadi hii ni ndogo sana kulinganisha na wasafiri **3,849** waliochanjwa katika kipindi kama hiki mwaka 2019/2020. Hii imetokana na kupungua sana kwa idadi ya wasafiri kutokana na janga la ugonjwa wa Korona linaloendelea ulimwenguni.

49. Mheshimiwa Spika, jumla ya kontena **23** zikiwemo za nguo, Televisheni, viatu na majokofu zilizoingia nchini zimekaguliwa na kufanyiwa ufukizaji. Aidha, Wizara kuitia kituo chake kilichopo Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume imefanya uhakiki wa vyeti **16,002** vya Korona kwa wasafiri, ambapo jumla ya vyeti **14,450** sawa na asilimia (90.3) vilikuwa vyeti halali na vyeti **202** sawa na asilimia (1.3) viligundulika kuwa vyeti bandia. Wahusika wa vyeti bandia wamefikishwa kwenye vyombo vya sheria. Jumla ya wafanyakazi **16** wa Bandari ya Malindi na **31** viwanja wa ndege (Unguja na Pemba) walipatiwa mafunzo juu ya kukabiliana na maradhi ya Korona.

Huduma za Afya ya Wafanyakazi

50. Mheshimiwa Spika, jumla ya wananchi **12,339** wakiwemo wafanyakazi wa Serikali, taasisi binafsi, wanafunzi na wafanya biashara za vyakula wamepimwa afya zao. Kati yao, **279** wameonekana kuwa na matatizo ya kiafya yakiwemo maambukizi ya mkojo (UTI), shindikizo la damu, minyoo, homa ya Ini “B”na “C”, homa ya matumbo, maradhi ya ngozi, pumu, kisukari, ajali na uoni hafifu. Wote waliobainika kuwa na matatizo walipatiwa ushauri wa kiafya na maelekezo stahiki.

Huduma za Afya ya Msingi ya Akili

51. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya imeendelea kutoa huduma za Afya za msingi ya Akili katika jamii pamoja na kusimamia haki na ustawii wa watu wenyewe matatizo ya Afya ya Akili. Jumla ya vituo **32** vya daraja la pili na hospitali za wilaya zilifanyiwa ukaguzi wa kuangalia utoaji wa huduma za akili. Miiongoni mwa kasoro zilizobainika ni upungufu wa baadhi ya dawa za kutibu ugonjwa wa akili na wataalam wa afya katika vituo vya kutolea huduma. Wizara inaendelea kuchukua hatua za kuondosha kasoro hizo.

PROGRAMU YA TIBA

- 52. Mheshimiwa Spika,** progamu hii ina husika na kusimamia utoaji wa huduma katika hospitali za vijiji (Vitongoji na Micheweni), Hospitali za Wilaya; Kivunge na Makunduchi kwa Unguja na Chake Chake, Wete kwa Pemba pamoja na Hospitali ya Mkao ya Abdulla Mzee. Aidha, inahusika na utoaji wa huduma kupitia Mpango wa Damu salama, Ushauri kwa Hospitali Binafsi, uchunguzi wa maradhi na kusimamia uendeshaji wa shughuli za mabaraza ya kitaaluma (madaktari, wauguzi na maabara) na huduma za Mkono kwa Mkono. Huduma hizi zinatolewa kupitia program ndogo ya huduma za matibabu na huduma za uchunguzi.
- 53. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, programu ya Tiba ilipangiwa shilingi **51,258,210,000**; hadi kufikia Machi 2021 shilingi **20,436,395,147** (asilimia 39.9) ziliingizwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:-
- i. Kuendelea na ujenzi wa Hospitali ya Kisasa ya Kufundishia Binguni;
 - ii. Kuanza ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika Hospitali ya Abdulla Mzee;
 - iii. Ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika Hospitali ya Kivunge;
 - iv. Kuendelea na ujenzi wa wodi ya wazazi Hospitali ya Chake Chake;
 - v. Kufanya ukarabati wa Hospitali ya Wete;
 - vi. Ununuzi wa dawa na vifaa Tiba; na
 - vii. Kukamilisha maabara ya Chakula, Dawa na Vipodozi.

Programu Ndogo Huduma za Matibabu

54. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matibabu, jumla ya wagonjwa **23,466** walilazwa kwa ajili ya kupatiwa matibabu (in-patients) na wagonjwa **319,693** walitibiwa matibabu ya nje (out-patient) kuititia kliniki za maradhi mbali mbali katika hospitali za Abdulla Mzee, Chake Chake, Wete, Kivunge, Makunduchi, Micheweni na Vitongoji. Pia, wagonjwa **309** walipatiwa rufaa kwenda Hospitali ya Mnazi Mmoja. Katika kipindi hicho wagonjwa 218 walisafirishwa nje ya Zanzibar kwa ajili ya matibabu; wagonjwa **209** wamepelekwa Tanzania Bara na **tisa** (9) wamepelekwa nje ya Tanzania.

Huduma za Damu Salama

55. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huduma za tiba ya damu salama, jumla ya chupa za damu **10,129** zilikusanywa kutoka kwa wachangiaji wa hiari; idadi hii ni sawa na asilimia **80.5** ya lengo la ukusanyaji wa damu lililowekwa. Damu zilizokusanywa zilifanyiwa uchunguzi wa magonjwa ya VVU, kaswende na Homa ya Ini B&C. Jumla ya chupa **9,372** za damu safi zilisambazwa katika hospitali za serikali na binafsi kwa Unguja na Pemba zinazotoa tiba za damu.

Huduma za Mabaraza ya Kitaaluma

56. Mheshimiwa Spika, katika kusimamia ufanisi wa utendaji katika hospitali za binafsi, Wizara kuititia Bodi ya ushauri wa hospitali binafsi ilifanya ukaguzi katika hospitali **36**, kati ya hizo tatu (**3**) zilisimamishwa kutoa huduma kutohakana na kasoro mbali mbali

zilizoonekana wakati wa ukaguzi; mapungufu yaliyobainika ni kutokuwa na wafanyakazi wenyе sifa za utabibu na mazingira yasiyoridhisha ya kutolea huduma za afya. Aidha, hospitali nyengine tatu **(3)** zimepewa barua za onyo na kutakiwa kurekebisha upugufu uliyojitokeza.

- 57. Mheshimiwa Spika**, kupitia Baraza la Wauguzi na Wakunga Zanzibar, jumla ya Wauguzi na Wakunga 1,802 wanaofanya kazi Zanzibar wamefanyiwa usajili na kupatiwa leseni. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021 jumla ya wauguzi **510** wamepatiwa leseni kati yao wauguzi 177 ni marudio (renew) na wauguzi 333 wapya baada ya kufanyiwa usajili. Aidha, Baraza limeendelea na shughuli za kusimamia maadili ya uuguzi na ukunga na kutoa miongozo ya utendaji. Baraza la Madaktari limesajili na kuwapa leseni madaktari bingwa wapya **19** (wazalendo - 11 na wa kigeni - 8) na wa marudio **33** (wazalendo - 27 na wakigeni 6). Aidha, madaktari wa kawaida **97** walisajiliwa na kupewa leseni. Kati yao wazalendo **91** na wa kigeni sita **(6)**.

Huduma za Vituo vya Mkono kwa Mkono

- 58. Mheshimiwa Spika**, vituo vya mkono kwa mkono vina jukumu la kuratibu na kusimamia masuala yote ya udhalilishaji. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021 vituo vya Mkono kwa Mkono vimepokea na kutoa huduma kwa wahanga wa udhalilishaji **1,480** kwa Unguja na Pemba. Matukio makuu yaliyori potiwa yanajumuisha kubakwa, jaribio la kubakwa na mimba za utotoni.

- 59. Mheshimiwa Spika**, wizara imetoa mafunzo ya utoaji wa rufaa kwa wahanga wa udhalilishaji kwa watendaji **sita** (6) wa vituo vya mkono kwa mkono. Mafunzo hayo yalijumuisha washauri nasaha **wawili** (2) na maafisa ustawi **wanne** (4). Aidha, mafunzo juu ya miongozo ya utowaji wa huduma (Standard Operating Procedures), yalitolewa kwa watendaji wote wa vituo vya mkono kwa mkono. Mafunzo yote haya yamelenga kuwasaidia watendaji kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Huduma ya Upatikanaji, Uhifadhi na Usambazaji wa Dawa na Vifaa vya utibabu

- 60. Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea na jitihada za kuimarisha huduma za afya kwa kuhakikisha upatikanaji mzuri wa dawa muhimu, vifaa tiba na uchunguzi kwa hospitali na vituo vya afya Unguja na Pemba. Katika kipindi cha Julai - Machi 2021, jumla ya shilingi **7,867,884,891** sawa na asilimia **46.3** ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa vya utibabu zimepatikana kutoka Serikalini. Aidha, Wizara imepokea dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi **8,476,207,381** kutoka kwa washirika wa maendeleo (**Kiambatisho namba 3a**).
- 61. Mheshimiwa Spika**, zoezi la kufanya makisio ya mahitaji ya dawa na vifaa (quantification) kwa mwaka wa fedha 2021/2022 limefanyika, ambapo jumla ya shilingi **bilionti 60.1** zinahitajika kukidhi mahitaji halisi ya ununuzi wa dawa na vifaa. Makisio hayo yamelenga kuimarisha maeneo kumi na saba (17) ya huduma, mchanganuo wake umewekwa katika **Kiambatisho namba 3b**.

Mahitaji hayo ya fedha kwa ununuzi wa dawa ni makubwa ukilinganisha na bajeti ya shilingi **bilioni 21.2** iliyotengwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

62. Mheshimiwa Spika, katika hatua nyengine, Wizara imefanya mapitio ya mfumo wa upatikanaji, uhifadhi na usambazaji wa dawa na vifaa vya utibabu (*Zanzibar Supply Chain Holistic Review*) katika hospitali, vituo vya afya pamoja na maeneo yote ya huduma za dawa. Zoezi hili litasaidia kuibua changamoto zilizopo za upatikanaji wa dawa ili ziweze kupatiwa ufumbuzi wa kuimarisha mfumo mzima wa huduma za dawa nchini.

Huduma za Tiba Asili na Tiba Mbadala

63. Mheshimiwa Spika, huduma za tiba za asili na tiba mbadala zinatekelezwa kwa kupitia Sheria namba. 8 ya mwaka 2008 iliyounda Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala, ambalo lina jukumu la kusimamia shughuli zote za waganga wa tiba asili/jadi na tiba mbadala kwa ajili ya kusaidia maendeleo ya dawa za miti shamba na kuweka viwango vya matumizi ya dawa kwa lengo la kuilinda jamii kutokana na matumizi mabaya ya dawa asili.

64. Mheshimiwa Spika, kupitia Baraza hili shughuli za kuelimisha jamii juu ya matumizi bora ya dawa za asili zilifanyika, sambamba na kufanya ukaguzi kwa wadau waliosajiliwa. Taaluma juu ya matumizi na uendeshaji wa huduma hizi zimeendelea kutolewa kwa wanaotoa huduma za tiba asili katika maeneo yasiyo rasmi; kama misikitini, masokoni, pembezoni mwa barabara na maeneo mengine yenye mikusanyiko ya watu. Katika kipindi

kinachoripotiwa waganga wapya **17** na wasaidizi waganga tisa (**9**) wamesajiliwa pamoja na usajili wa Klinik **2** na Maduka ya dawa asili **10**. Idadi hii inafanya jumla ya waganga waliosajiliwa kufikia **460**, waganga wasaidizi **147**, kliniki za tiba asili **37**, Tiba mbadala nne na Maduka ya dawa asili **156**.

Programu Ndogo Huduma za Uchunguzi

- 65. Mheshimiwa Spika**, ni dhahiri kwamba huduma bora za matibabu zinahitaji uchunguzi sahihi. Kwa kulizingatia hilo, Wizara imeendelea kutoa huduma za uchunguzi kwa kadri ilivyowezekana kupitia vipimo mbali mbali vya uchunguzi wa maradhi, bidhaa na kemikali. Kwa kipindi cha utekelezaji, jumla ya vipimo vya kimaabara **203,016** na vipimo vya mionzi **34,756** (Xray/CT Scan - 18,554 na Ultra Sound - 16,202) vilifanyika.

Huduma za Chakula, Dawa na Vipodozi

- 66. Mheshimiwa Spika**, Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi ni Taasisi yenye jukumu la kusimamia na kudhibiti usalama, ubora na ufanisi wa chakula, dawa, vipodozi, vifaa tiba na reajenti. Taasisi hii inatekeleza shughuli zake kwa mujibu wa Sheria Nam. 2 ya mwaka 2006 ya Chakula, Dawa na Vipodozi na marekebisho yake ya Sheria Nam. 3 ya mwaka 2017.
- 67. Mheshimiwa Spika**, jumla ya maeneo **2,823** (asimilia 83) ya biashara za chakula (1,755), dawa (733), vipodozi (317) na vifaa tiba (18) yamefanyiwa ukaguzi. Katika ukaguzi huo maeneo **42** yalizuiliwa kuendelea na biashara kutokana na kutokidhi vigezo

vilivyowekwa. Aidha, tani **1,571.13** za bidhaa zisizofaa kwa matumizi ya binadamu zilikamatwa; ambapo tani **590.56** (chakula 560.56, dawa 35 na vipodozi 7) zimeteketezwa na tani **956.57** zimerudishwa sehemu zilikotoka.

- 68. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa usajili, jumla ya maeneo **1,892** (chakula 1,087, dawa 475, vifaa vya utibabu 25 na vipodozi 305), ambayo ni sawa na asilimia **63** ya maeneo **3,000** yaliyopangwa ya biashara/uzalishaji wa bidhaa yamefanyiwa tathmini na kusajiliwa. Vile vile, maombi **162** ya usajili wa bidhaa yalipokelewa, ambapo bidhaa **120** (chakula 112, dawa 2 na vifaa vya utibabu 6) zimesajiliwa baada ya kufanyiwa tathmini na kukidhi vigezo vilivyowekwa. Aidha, jumla ya sampuli **1,374** zikiwemo za dawa **7**, chakula **1,286**, vipodozi **78** na vifaa tiba **2** zilifanyiwa uchunguzi; sampuli **146** (chakula 133, dawa 4 na vipodozi 9) hazikufikia viwango.

Huduma za Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali

- 69. Mheshimiwa Spika**, Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ina jukumu la kutoa huduma za kitaalamu na za kisayansi kwa kufanya uchunguzi wa vielelezo vinavyowasilishwa kutoka Taasisi mbali mbali. Vielelezo hivyo vinahusisha Makosa ya Jinai, Vinasaba, Sumu pamoja na Chakula. Pia ina jukumu la kudhibiti kemikali kwa kufanya ukaguzi na usajili wa kemikali, wahusika wa ununuizi na utunzaji pamoja na majengo yanayotumika kuhifadhi kemikali.

- 70. Mheshimiwa Spika**, jumla ya vibali **1,785** vimetolewa kwa wafanyabiashara wanaoshughulika na uingizwaji wa kemikali. Vile vile, majengo **80** ya kuhifadhia kemikali yamesajiliwa pamoja na kufanya ukaguzi katika maeneo **142**. Pia, sampuli **1,147** zimepokelewa na kufanyiwa uchunguzi; sampuli hizo ni pamoja na zilizohusiana na makosa ya jinai (dawa za kulevyta, bangi, pombe ya kienyeji), vinasaba (DNA), chakula na nyenginezo.

PROGRAMU YA HIFADHI YA JAMII, MAENDELEO YA JINSIA NA WATOTO

Programu Ndogo ya Hifadhi ya Jamii

- 71. Mheshimiwa Spika**, shughuli za hifadhi ya jamii zinatekelezwa kwa kuzingatia Mikakati ya Kitaifa, Sheria ya Watoto Nam. 6 ya 2011 na Sera ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2014. Kwa mwaka wa fedha 2020/2021, ilitengewa shilingi **11,553,794,096**; ambapo hadi kufika Machi 2021 shilingi **6,412,830,755** sawa na asilimia **55.5** zimeingizwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:-
- Kukuza usawa wa kijinsia, kumuwezesha mwanamke na kuendeleza mapambano ya kumaliza vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto; na
 - Kuimarisha uratibu wa hifadhi ya jamii na hifadhi ya mtoto.
- 72. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha Mfumo wa Hifadhi ya Mtoto, Wizara imeendelea kupokea malalamiko ya ukiukwaji wa haki za watoto na kuyafanyia kazi. Jumla ya malalamiko **508** (Unguja - 251 na Pemba - 257) yamepokelewa; kati ya hayo, **347** yalihuisha watoto kunyimwa matunzo (Unguja -139 na Pemba - 208) na **161** ya mvutano wa malezi. Malalamiko **333** yalipatiwa ufumbuzi na malalamiko **76** yalitolewa rufaa kwenda Mahakamani, wahusika **81** walikubaliana kifamilia na **18** yanaendelea na hatua. Katika migogoro hiyo watoto **1,074** (wanawake - 512 na wanaume - 562) wa familia hizo waliathirika. Jumla ya kesi za jinai na madai **327** zimesikilizwa mahakamani zikiwemo kesi **65** za madai kutoka Unguja na kesi za jinai **262** (Unguja -123 na Pemba -139). Kesi **10** za madai na kesi nne (4) za jinai zimeshatolewa hukumu.

- 73. Mheshimiwa Spika**, jumla ya watoto **34** (wanawake - 17 na wanaume - 17) wanaendelea kutunzwa katika nyumba ya watoto iliopo Mazizini na wahanga **26** (wanawake - 18 na wanaume - 8) wamepatiwa hifadhi ya muda katika Nyumba Salama. Pia, watoto **19** (wanawake – 2 na wanaume - 17) wanaokinzana na sheria wamepokelewa katika Kituo cha Marekebisho ya Tabia. Watoto hawa hupatiwa taaluma za stadi za maisha zikiwemo ufundi, ushoni, uchoraji pamoja na kupatiwa ushauri nasaha. Katika hatua nyengine, jumla ya vituo saba (7) (Unguja - 6 na Pemba - 1) vya jamii vinavyotoa huduma za malezi kwa watoto vimefuatiliwa kwa lengo la kuhakikisha watoto wanakuwa kwenye mazingira salama wanapokuwa vituoni humo.
- 74. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuwatunza wazee **80** kwa kupatiwa huduma muhimu katika Makaazi ya Wazee Unguja na Pemba. Kituo cha Welezo kina wazee **41** (wanawake -11 na wanaume - 30), Sebleni **30** (wanawake - 19 na wanaume - 11) na Limbani **9** (wanawake - 3 na wanaume - 6).
- 75. Mheshimiwa Spika**, huduma za malipo ya Pensheni Jamii kwa wazee wenye umri wa miaka 70 na kuendelea zimeendelea kutolewa, ambapo jumla ya wazee **29,061** (Unguja - 17,989 na Pemba - 11,072) wamesajiliwa; kati yao, wazee **2,365** (Unguja - 1,458 na Pemba - 907) wamesajiliwa katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021. Katika kipindi hicho wazee **1,801** (Unguja - 1,141 na Pemba - 660) wamefariki dunia, Mwenyezi Mungu awarehemu, Amin!

- 76. Mheshimiwa Spika**, familia **160** (Unguja - 91 na Pemba - 69) zenyewe watoto wanaoishi katika mazingira magumu na mama **15** (Unguja - 11 na Pemba - 4) waliojifungua zaidi ya mapacha wawili walipatiwa msaada wa kiustawi. Vile vile, waathirika wa maradhi ya ukoma **52** wanaoishi katika Kijiji cha Makundeni walipatiwa posho za kujikimu. Sambamba na huduma hizo pia, wizara imezika maiti **16** zisizokuwa na wenyewe.
- 77. Mheshimiwa Spika**, wizara inatoa malipo ya fidia kwa wafanyakazi wanaopata ajali kazini; kwa kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021 madai **67** ya fidia yenye thamani ya shilingi **121,026,355** yalipokelewa (Unguja - 55 na Pemba -12). Madai **10** yenye thamani ya shilingi **2,598,000** yamelipwa (Unguja - 8 na Pemba - 2); madai **57** (Unguja - 47 na Pemba - 10) yenye thamani ya shilingi **118,428,297** yanashubiri kulipwa na madai **16** yanaendelea kufanyiwa taratibu za tathmini.

Programu Ndogo ya Maendeleo ya Jinsia na Watoto

- 78. Mheshimiwa Spika**, programu hii ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa haki za wanawake na watoto na inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sera na Mipango ya Kitaifa, Mikataba ya Kikanda na Kimataifa inayowahusu wanawake na watoto. Shughuli zilizopangwa kutekelezwa na programu hii zinajumuisha:-
- i. Kuelimisha jamii juu ya haki za wanawake na watoto na kuwahamasisha kuchukua hatua katika kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji katika maeneo yao;

- ii. Kuendelea na uratibu wa Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kupambana na Vitendo vya Ukatili na Udhaliishaji wa Wanawake na Watoto;
 - iii. Kuwawezesha na kuwajengea uwezo waratibu wa wanawake na watoto wa shehia;
 - iv. Kutoa taaluma kwa wanafunzi wa skuli mbali mbali juu ya kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia;
 - v. Kuendelea kuimarisha Mabaraza ya Watoto na Vilabu vya Skuli katika kujikinga na kuripoti matukio ya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto;
 - vi. Kuimarisha uwajibikaji na malezi bora kwa watoto; na
 - vii. Kuimarisha mfumo wa upokeaji na utoaji wa taarifa za matukio ya ukatili na udhalilishaji wa watoto kuitia nambari ya simu 116.
- 79. Mheshimiwa Spika,** Wizara kuitia programu hii imeendelea kuhamasisha jamii juu ya kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto katika shehia **81** (Unguja - 45 na Pemba - 36) kuitia midahalo na magari ya matangazo. Aidha, Wizara imeendesha programu maalum ya uelimishaji na uhamasishaji wanafunzi na walimu juu ya kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji, ambapo skuli **127** (Unguja - 81 na Pemba - 46) zimefikiwa. Kuitia programu hizo, wananchi wakiwemo wanafunzi wameweza kuibua sababu na maeneo hatarishi yanayochangia ongezeko la vitendo hivyo pamoja na kupanga mikakati ya utekelezaji wake.

- 80. Mheshimiwa Spika**, viongozi wa dini wamekuwa na mchango mkubwa katika kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Kwa mantiki hiyo, Wizara imezipatia usafiri na vifaa timu 11 za wilaya za viongozi wa dini kwa ajili ya kutoa elimu na kuihamasisha jamii juu ya kupambana na vitendo hivyo. Uhamasishaji huu hutolewa kupitia mihadhara, khutba, vyombo vya habari na kutoa taaluma katika mikusanyiko mbali mbali ya waumini. Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wananchi pamoja na viongozi wa dini kwa kuchukua hatua mbali mbali katika kujikinga na vitendo hivi visiendelee kutokea katika jamii yetu.
- 81. Mheshimiwa Spika**, kupitia programu hii watendaji **26** kutoka Pemba (wanawake - 20 na wanaume - 6) walipatiwa vifaa pamoja na mafunzo ya utoaji wa huduma za ushauri nasaha ikiwemo msaada wa kisaikolojia kwa wahanga wa vitendo hivyo. Aidha, mafunzo ya usimamizi na jinsi ya utoaji wa huduma yalitolewa kwa waratibu **168** (wilaya za Pemba - 129 na wilaya ya Kaskazini "A" - 39). Kufuatia mafunzo hayo, waratibu wameanza kuchukua hatua za kusimamia mabaraza ya watoto na kufuatilia matukio ambapo wahanga **326** (Unguja - 231 na Pemba - 95) pamoja na familia zao wamefuatiliwa na hatua muafaka zilichukuliwa.
- 82. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hiki cha utekelezaji, Wizara ilipokea malalamiko **167** (Unguja - 93 na Pemba - 74). Malalamiko hayo yalihusu kutelekezwa na mume, mgawanyo wa mali walizochuma wanandoa, madai ya mahari, talaka, mimba nje ya ndoa, kupigwa, pamoja na shambulio la matusi. Malalamiko yote yanayohusu madai yalipatiwa ufumbuzi na ya jinai yalipelekwa katika ngazi za kisheria.

- 83. Mheshimiwa Spika**, vikundi **25** (Unguja - 16 na Pemba - 9) vya wanawake wajasiriamali vikiwemo vikundi vinne (4) vya wajasiriamali wenye ulemavu vimetembelewa na kupewa ushauri na maelekezo katika utekelezaji wa shughuli zao; shughuli zinazofanywa na vikundi hivyo ni pamoja na ufumaji, ushoni, biashara za nguo na uvuvi wa chaza. Aidha, kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji vikundi hivyo vilipatiwa mikopo kwa ajili ya kuimarisha biashara zao za kiuchumi.
- 84. Mheshimiwa Spika**, mabaraza ya watoto ya shehia **45** za Wilaya ya Kaskazini 'A', **32** za Wilaya ya Kaskazini "B" na **mbili** (2) za Wilaya ya Mkoani yamepatiwa mafunzo ya uendeshaji wa mabaraza, kutambua haki na wajibu wa mtoto na namna ya kujikinga na vitendo vya ukatili na udhalilishaji. Vile vile, jumla ya skuli **18** zimepatiwa mafunzo ya kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto; Wilaya ya Chake Chake (**4**), Wete (**6**), Mkoani (**4**), na Micheweni (**4**). Aidha, wazazi **1,200** kutoka Shehia **10** za Wilaya ya Kaskazini 'A' wenye watoto katika mabaraza ya watoto ya shehia wamepatiwa taaluma juu ya usimamizi bora wa mabaraza hayo katika shehia zao.

PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA

85. Mheshimiwa Spika, program hii unahusika na masuala ya rasilimali watu ikiwemo ajira, kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia nafasi za masomo pamoja na stahiki zao. Aidha, ina jukumu la kuandaa na kusimamia sera, miongozo, mipango pamoja na kuratibu taarifa za afya. Kwa mwaka 2020/2021, jumla ya shilingi **20,312,959,000** zilitengwa; hadi kufikia Machi 2021 **shilingi 14,128,406,548** (asilimia 69.6) zilitumika kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:-

- i. Kupeleka masomoni wafanyakazi wa kada zilizopewa kipaumbele kwa mujibu wa mahitaji;
- ii. Kufanya malipo ya mishahara kwa watendaji wa idara ya uendeshaji na mipango;
- iii. Kutayarisha mpango wa ufuutiliaji na tathmini wa mpango mkakati wa nne wa afya;
- iv. Kuimarishe mifumo ya taarifa; na
- v. Kuratibu shughuli za uandaaji wa sera, mipango, tafiti na taarifa mbali mbali za Wizara.

Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji

86. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki cha utekelezaji Wizara imeajiri wafanyakazi **1,073** (Unguja - 853 na Pemba - 220), wakiwemo madaktari (26), wauguzi (144), wafamasia (9) kama walivyorodheshwa katika **Kiambatisho namba 4**. Pia, wafanyakazi **67** wamerudi kutoka masomoni. Katika kuhakikisha kwamba

kunakuwa na wataalamu wa kutosha, jumla ya wafayakazi **151** wamepelekwa masomoni wakiwemo madaktari bingwa **48** (**Kiambatisho namba 5(a) na 5(b)**). Idadi hii inafanya jumla ya wafanyakazi **425** wanaoendelea na masomo ndani na nje ya nchi. Hadi kufikia Machi 2021, idadi ya madaktari wazalendo imefikia **371** na wauguzi **1,488**; idadi hii inafanya daktari mmoja kuhudumia watu **4,630** (1:4,630) na muuguzi mmoja kuhudumia watu **1,154** (1:1,154). Katika kipindi hicho, wafanyakazi **31** wamestaafishwa kwa mujibu wa taratibu za kiutumishi na wafanyakazi saba (**7**) wamefariki dunia; Mwenyezi Mungu azihifadhi roho zao mahali pema Peponi, Amin.

- 87. Mheshimiwa Spika**, Wizara ilifanya ufuatiliaji wa wafanyakazi waliopo masomoni katika vyuo vya Tanzania Bara ili kuja maendeleo ya masomo yao. Jumla ya wafanyakazi **57** wanaosoma Muhimbili University of Health and Allied Sciences (MUHAS), Catholic University of Health and Allied Sciences (CUHAS), University of Dodoma (UDOM) na Kilimanjaro Christian Medical University College (KCMUCO- Moshi) walifuatiliwa. Ufuatiliaji huo ulibaini kwamba wafanyakazi wote wanaoendelea na masomo kulingana na fani walizochagua awali.
- 88. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha wafanyakazi wanapata maslahi na stahiki zao kwa mujibu wa taaluma zao, Wizara imewasilisha Kamisheni ya Utumishi mapendekezo ya Muundo wa Utumishi “Scheme of Services” pamoja na stahiki nyengine kwa utekelezaji. Ni matumaini ya Wizara kwamba utekelezaji wa muundo huo utapunguza malalamiko ya wafanyakazi.

- 89. Mheshimiwa Spika**, Wizara imesaini Hati za Makubaliano (MoU 3, na Mikataba 63 ikiwemo ya ununuzi wa dawa na vifaa vya utibabu, vifaa, huduma na ujenzi. Pia, kanuni 11 za Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi (ZFDA) zimeandaliwa kwa kuwekwa masharti bora ya utekelezaji wa Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya mwaka 2006 (na Marekebisho ya 2017). Kanuni hizo tayari zinafanya kazi.

Programu ndogo Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara

- 90. Mheshimiwa Spika**, Wizara kuitia programu hii imekamilisha rasimu ya pili ya kitita cha huduma za afya “Essential Health Care Package” kwa ngazi zote za utoaji huduma za afya. Vile vile, Rasimu ya mwisho ya Mpango Mkakati wa Nne wa Wizara umekamilika, ambapo shughuli za utekelezaji mpango huo zimezingatiwa katika bajeti hii. Aidha, hadidu rejea kwa ajili ya kufanya Mapitio ya Sera ya Afya ya mwaka 2011 zimetayarishwa, mshauri mwelekezi tayari amepatikana na kazi itaanza muda wowote kuanzia sasa.
- 91. Mheshimiwa Spika**, miongozo mbali mbali imetayarishwa ikiwemo ya kusimamia viwango vya utoaji wa huduma na kufanya ukaguzi, miongozo ya jinsi ya kujikinga na maambukizi (IPC) kwa wafanyakazi na wagonjwa. Miongozo mingine iliyotayarishwa ni wa utayarishaji wa bajeti kwa kazi ambazo zinagharamiwa na Mfuko wa Pamoja wa Fedha (Basket Fund), muongozo huo umetumika katika kutayarisha mipango kazi na bajeti kwa mwaka

2021/2022. Shughuli nyengine zilizotekelawa ni kufanya mapitio ya utekelezaji wa mpango kazi wa mwaka 2020/2021 kwa timu za afya za halmashauri pamoja na hospitali za Unguja na Pemba, ambazo zinazopata ufadhilli kuitia Mfuko wa Pamoja wa Fedha. Changamoto zilizobainika katika mikutano hiyo zimesaidia katika kuibua vipaumbele vya bajeti ya mwaka 2021/2022.

92. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea na zoezi la kufanya tathmini ya shughuli za ufuatiliaji na tathmini (Monitoring & Evaluation), ambapo ukusanyaji wa taarifa umekamilika na ripoti iko tayari. Kupitia program hii, Wizara imetayarisha taarifa mbali mbali za utekelezaji wa mpango kazi za mwaka na robo mwaka; taarifa za utekelezaji miradi ya maendeleo; na taarifa za Kamati za Baraza la Wawakilishi pamoja na Hotuba hii ya Bajeti ya mwaka 2021/2022, ambayo leo ninaisoma mbele ya Wajumbe wa Baraza hili. Taarifa nyengine zilizotayarishwa ni utekelezaji wa ilani na maagizo ya serikali na Kitabu cha Taarifa za Afya kwa mwaka 2019 (Health Information Bulletin).
93. **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarishe mashirikiano na wadau mbali mbali wa sekta ya afya, wizara ilifanya mkutano wa Kamati ya pamoja na washirika wa maendeleo (*Sector Wide Approach Steering Committee*). Mkutano huo ulijadili masuala mbali mbali yanayohusu sekta ya afya hapa nchini. Miiongoni mwa maazimio yaliyofikiwa ni kufanya mapitio ya mkataba wa makubaliano ya mfuko wa “Basket Fund” pamoja na kuwashirikisha wadau katika hatua za awali za kutayarisha mpango kazi.

94. Mheshimiwa Spika, Wizara pia, ilifanya mkutano na taasisi ya “Mkapa Foundations” kwa ajili ya kubainisha maeneo ya uimarishaji wa mfumo wa utoaji wa huduma za afya, ambayo taasisi hiyo inaweza kusaidia. Maeneo hayo yalihusu uimarishaji wa nguvu kazi ya afya, mikakati ya kupata vyanzo mbadala vya kugharamia huduma za afya na uimarishaji wa utoaji wa huduma za afya katika jamii (community interventions). Aidha, Kamati Kiongozi sambamba na Kamati ya Kitaalamu inayojumuisha Makatibu Wakuu na wataalamu kutoka ngazi husika wameanza hatua za awali za matayarisho ya uanzishwaji wa Mfuko wa Bima ya Afya Zanzibar.

Taasisi ya Utafiti wa Afya Zanzibar

95. Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana na taasisi za ndani na nje ya Zanzibar zikiwemo Shirika la Afya Ulimwenguni, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji na Mifugo pamoja na Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, taasisi imefanya utafiti wa ugonjwa juu ya kinga ya maradhi ya Korona katika jamii (Sero Epidemiological Investigation of Korona in Zanzibar), utafiti wa kuangalia ufuatiliaji wa miongozo na kupata maoni ya wananchi juu ya ugonjwa wa Korona (Compliance of Public Health Measures to Interupt with Covid - 19 Transimission in Zanzibar). Aidha utafiti wa kutambua miti ya dawa inayotumika kwa matibabu ya njia za hewa Zanzibar umefanyika. Jumla ya maandiko ya tafiti (Research Proposals) 96 yamepitiwa na kuidhinishwa, 17 kutoka taasisi za serikali na binafsi (orodha ya majina yanaonekana katika **Kiambatisho namba 6**) na 79 ni tafiti za wanafunzi.

96. Mheshimiwa Spika, ujenzi wa maabara mbili za taasisi “Microbiology na Molecular” umekamilika. Aidha, matayarisho ya ujenzi wa maabara itakayotumika kwa shughuli za “Biochemistry” unaendelea. Sambamba na hayo, ujenzi wa jengo la utawala uko katika hatua za mwisho. Taasisi imeendelea kuwa na mashirikiano na mahusiano na taasisi zingine ndani na nje ya nchi kwa kubadilishana maarifa na ujuzi. Taasisi hizo ni pamoja na NIMR, COSTECH, IHI, SUZA, ZFDA, ZBS, MMH, ZALIRI, na Tiajin University ya China.

Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Afya Pemba

97. Mheshimiwa Spika, programu hii inahusika na uratibu wa shughuli zote za afya kwa upande wa Pemba. Programu hii imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa malengo ya Wizara yaliyowekwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Jumla ya shilingi **8,796,493,000** zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zake. Hadi kufikia Machi, 2021 shilingi **7,844,780,433** ziliingizwa sawa na asilimia **89.1** ya fedha zote zilizotengwa kwa mwaka 2020/2021.

98. Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021 programu hii imetua mafunzo ya kujikinga na maambukizo ya maradhi “Infection Prevention and Control” kwa wafanyakazi **35** wa Hospitali ya Chake Chake. Matengenezo madogo madogo yamefanyika yakiwemo ya jengo la kutolea huduma za dharura katika Hospitali ya Abdulla Mzee, jengo la kutolea huduma za

matibabu ya nje, jengo la maabara, pamoja na ujenzi wa uzio katika Hospitali ya Chake Chake. Shughuli nyengine zilizofanywa ni pamoja na ununuzi wa vifaa vya utibabu; vikiwemo mashine za kupimia shindikizo la damu, vifaa vya kidijitali vya kupimia joto la mwili pamoja na “reagents” kwa ajili ya uchunguzi wa kimaabara kwa hospitali za Micheweni na Vitongoji.

PROGRAMU YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA (H02)

99. Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Mnazi Mmoja inatambuliwa kuwa Wakala wa Serikali kufuatia kupitishwa kwa Sheria Nam. 3 ya mwaka 2016. Hospitali hii ndio pekee hapa Zanzibar inayotoa huduma za rufaa kupitia Bodi ya Ushauri ya Hospitali ikiwa na lengo la kuimarishe huduma za uchunguzi, matibabu, tafiti na kutoa mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi wa kada za afya. Utekelezaji wa shughuli za Programu ya Hospitali ya Mnazi Mmoja unafanyika kupitia programu ndogo mbili (2); programu ndogo ya huduma za uchunguzi na matibabu; na programu ndogo ya uongozi wa hospitali na utawala kama ifuatavyo:-

Programu Ndogo ya Uchunguzi na Matibabu

100. Mheshimiwa Spika, huduma za uchunguzi ni muhimu katika kutoa matibabu sahihi kwa mgonjwa. Katika kipindi hiki cha utekelezaji, vipimo vya maabara **153,502** na vipimo **34,490** kwa njia ya picha (Ultrasound - 15,652; X-ray - 13,702; MRI -1,325; na CT Scan - 3,811) vilifanyika. Katika kuhakikisha hospitali inaimarisha huduma za uchunguzi kwa kutumia vifaa bora; katika kipindi cha Julai, 2020 - Machi 2021, hospitali imefunga mashine mpya ya uchunguzi wa maradhi ya Korona, ambayo inatumika katika kufanya uchunguzi wa maradhi hayo.

101. Mheshimiwa Spika, katika kuimarishe huduma za matibabu, Wizara inaendelea kutoa huduma mbali mbali ikiwemo huduma za dharura, huduma za kliniki kwa maradhi maalum kama vile saratani, moyo, ngozi, mifupa na nyenginezo. Jumla ya wagonjwa

107,357 wastani wa wagonjwa **397** kwa siku walipatiwa huduma za matibabu ya nje (out-patient) na wagonjwa **73,967** (wanawake - 41,466 na wanaume 32,501) walilazwa kwa magonjwa tofauti. Aidha, wajawazito **13,876** walilazwa katika hospitali ya Mwembeladu na Mnazi Mmoja ambapo wajawazito **11,673** walijifungua kwa njia ya kawaida na **1,788** walijifungua kwa njia ya upasuaji sawa na asilimia **13**.

102. Mheshimiwa Spika, huduma za matibabu ya kusafisha damu (Dialysis) kwa wagonjwa wenyewe matatizo ya Figo zimetolewa, ambapo wagonjwa **38** wanaendelea kupatiwa huduma hiyo. Aidha, jumla ya wagonjwa wapya **223** walihudhuria katika kliniki ya Saratani kwa ajili ya kupatiwa huduma; saratani ya matiti inaonekana kuongoza kwa kuwa na wagonjwa **46** ikifuatiwa na saratani ya mlango wa kizazi ikiwa na wagonjwa **41**.

103. Mheshimiwa Spika, jumla ya wagonjwa **800** wamepatiwa matibabu katika kliniki maalum ya maradhi ya moyo, ambapo wagonjwa **215** ni wapya na wagonjwa **585** wa marejeo. Aidha, katika kuwapunguzia wananchi na Serikali gharama za matibabu nje ya nchi, hospitali imeendesha kambi **nane** (8) za uchunguzi wa watoto wenyewe matatizo na matibabu ya upasuaji. Wagonjwa **724** walifanyiwa uchunguzi, kati yao **561** sawa na asilimia **77** walifanyiwa upasuaji (Neurosurgery 70 na macho 491). Kambi hizi ziliendeshwa kwa mashirikiano ya pamoja na madaktari bingwa kutoka nchi za Uhispania na Israeli.

Programu Ndogo ya Uongozi wa Hospitali na Utawala

- 104. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha uwepo wa wafanyakazi wa kutosha, hospitali imepata wafanyakazi wapya **364** wakiwemo madaktari (9), wauguzi (9), mfamasia (1), afisa afya ya mazingira (19), afisa ushauri nasaha (10), afisa ustawi wa jamii (18) na wahudumu (293). Aidha, Hospitali imepokea madaktari bingwa **wawili** (2) wa watoto na daktari **mmoja** (1) wa magonjwa ya akili, ambao wamerejea kutoka masomoni.
- 105. Mheshimiwa Spika**, mionganini mwa mafanikio mengine ni kuendelea kwa mashirikiano na taasisi za kimataifa zikiwemo Hospitali ya Chuo Kikuu cha Haukeland ya Norway na Hospitali ya Chuo Kikuu cha Alexandria kupitia mashirikiano na “Nile Hope” ya Misri. Mashirikiano hayo yanajumuisha mafunzo, kubadilishana wataalamu na kufanya kambi za matibabu, upatikanaji wa vifaa tiba pamoja na kuimarisha miundombinu ya hospitali.
- 106. Mheshimiwa Spika**, mafunzo ya muda mfupi yenyeye lengo la kuthibitishwa kazini yametolewa kwa wafanyakazi **300** katika Chuo cha Utumishi wa Umma. Pia, mafunzo ya “quick book” yametolewa kwa wahasibu kwa lengo la kujengewa uwezo wa kutumia mfumo huo. Aidha, hospitali imefanya zabuni **tatu** (3) za ununuizi wa kitanda cha upasuaji kwa huduma za masikio, pua na koo “ENT”, Endoscopy kwa ajili ya uchunguzi na matibabu ya maradhi ya pua, koo na masikio pamoja na ununuizi wa kompyuta. Vile vile, hodhi la kuhifadhia ‘liquid oxygen’ katika hospitali ya Mnazi Mmoja limeunganishwa na paipu za kusafirishia na imeanza kutumika mawodini.

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

Ujenzi wa Maabara ya Uchunguzi ya Chakula, Dawa na Vipodozi

107. Mheshimiwa Spika, wizara imesimamia utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa jengo la Maabara ya kisasa ya Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi. Mradi huo unaendelea katika hatua ya umaliziaji wa jengo kwa uwekaji wa miundombinu ya maabara sambamba na uwekaji wa miundombinu ya umeme, vipoza hewa maalum vya maabara, gesi na mifumo ya mtandao. Ujenzi wa jengo hilo umewekewa jiwe la msingi na **Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid** tarehe 04 Januari, 2021 katika shamrashamra za kutimiza miaka 57 ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa sasa mradi huu umefikia asilimia **81** ya ujenzi.

Ujenzi wa Bohari ya Dawa Pemba

108. Mheshimiwa Spika, mradi huu wa ujenzi wa jengo la Bohari katika eneo la Hospitali ya Vitongoji Pemba pamoja na jengo la ofisi umeanza mwezi Machi 2019. Napenda kuwaarifu wajumbe wa Baraza lako kwamba ujenzi umekamilika na sasa shughuli za bohari zimeanza rasmi katika majengo hayo.

Ujenzi wa Hospitali ya Wagonjwa wa Akili

109. Mheshimiwa Spika, ujenzi wa hospitali hii ya kisasa ya ghorofa moja itakayokuwa na vitanda **100** unafadhiliwa kwa pamoja baina ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Haukeland University Hospital ya Norway kwa makubaliano ya kugharamia asilimia 50

kwa kila upande. Mradi umeanza mwaka 2018, utekelezaji wake umefikia asilimia 93, kwa sasa upo katika hatua za mwisho za kuunganisha mfumo wa umeme na uwekaji wa “solar”. Hospitali hii inatarajiwa kufunguliwa rasmi mwezi Agosti, 2021.

Ujenzi wa Maabara ya Uchunguzi wa Virusi - Binguni

110. Mheshimiwa Spika, kufuatia kuibuka kwa maradhi yanayosababishwa na virusi duniani, Serikali iliamua kujenga maabara ya uchunguzi wa virusi, ambayo pia itatumika kupima ugonjwa wa Korona. Ujenzi huo ulikabidhiwa kwa kampuni ya ujenzi ya Serikali na umefikia ghorofa ya pili. Hata hivyo, ujenzi huo umesita kutokana na ukosefu wa upatikanaji wa fedha.

Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa na Kufundishia - Binguni

111. Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya bajeti ya mwaka 2020/2021, tulieleza azma ya Serikali ya kuanza kwa ujenzi wa Hospitali ya rufaa na kufundishia katika eneo la Binguni, Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja. Kutokana na uhaba wa fedha, Serikali iliamua kuanza na ujenzi wa jengo la dharura, ambapo kazi iliyofanyika ni kuchimba msingi na kuzungushia mabati.

Ujenzi wa Wodi za Mama na Mtoto katika Hospitali ya Kivunge na Chake Chake

112. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha huduma za mama na mtoto zinatolewa katika hali ya kuridhisha, Wizara ilipanga kujenga wodi maalum kwa huduma hizo. Napenda kuchukuwa

fursa hii kuwaeleza wajumbe kwamba ujenzi wa wodi hizo katika Hospitali ya Kivunge umekamilika na kuanza kazi. Aidha, ujenzi wa ghorofa moja katika hospitali ya Wilaya ya Chake Chake unaendelea, umefikia hatua za kutandika jamvi la ghorofa ya kwanza.

Ukarabati mkubwa wa Hospitali ya Wete na Ujenzi wa Nyumba za Wafanyakazi katika Hospitali ya Mkoa ya Abdulla Mzee

113. Mheshimiwa Spika, ukarabati wa Hospitali ya Wete unatarajiwa kupata fedha za ufadhili kutoka Serikali ya Abudhabi, ambapo kwa sasa mazungumzo juu ya utekelezaji wa ujenzi huo yanaendelea. Kwa upande wa ujenzi wa nyumba za wafanyakazi wa Hospitali ya Abdulla Mzee tayari Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China wameshaiarifu wizara kupatikana kwa mkandarasi. Wizara tayari imeshaawandikia barua wakandarasi hao ili kuingia nchini na kuanza ujenzi huo.

CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA WAKATI WA UTEKELEZAJI

114. Mheshimiwa Spika, wizara imekabiliwa na changamoto mbali mbali wakati wa utekelezaji wa shughuli zake, zikiwemo: -

- i. Uchache wa wataalamu katika sekta ya afya hususan katika fani ya radiolojia, wataalamu wa usingizi, wahandisi wa vifaa tiba na wafamasia;
- ii. Upungufu wa vifaa vya utibabu wa mifupa;
- iii. Uhaba wa baadhi ya dawa; na
- iv. Kuharibika mara kwa mara mashine za uchunguzi kutokana na wingi wa wagonjwa.

115. Mheshimiwa Spika, jitihada zilizochukuliwa katika kutatua changamoto hizo ni pamoja na wizara kuongeza bajeti ya dawa na vifaa vya utibabu, kuajiri wataalamu wa afya pamoja na kuwatayarishia mazingira mazuri ya kazi. Vile vile, wizara imeandaa mpango wa kukiimarisha kitengo cha ufundi kwa ajili ya kufanya matengenezo ya vifaa katika hospitali na vituo vya afya.

MWELEKEO WA BAJETI NA VIPAUMBELE VYA WIZARA, 2021/2022

116. Mheshimiwa Spika, mwelekeo wa utekelezaji wa Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto katika mwaka wa fedha 2021/2022 umezingatia maelekezo ya Serikali ya awamu ya nane (8) katika kuimarisha utoaji wa huduma ili uendane na kauli mbiu ya CCM katika Uchaguzi Mkuu wa 2020 “**YAJAYO NI NEEMA TUPU**”. Hivyo, Wizara imejikita katika kutekeleza maagizo yaliyotolewa katika matukio mbali mbali ya kitaifa.

117. Mheshimiwa Spika, kufuatia maamuzi ya Serikali ya kurejeshwa huduma zilizogatuliwa katika sekta mama, Wizara itahakikisha kwamba huduma hizo zitaendelea kuimarishwa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa ya upatikanaji wa huduma bora za afya kwa wote (Universal Health Coverage). Vile vile, nguvu zaidi zitaelekezwa katika kupambana dhidi ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia na kustawisha jamii. Kwa muktadha huo, vipaumbele vya wizara vimezingatia mapendekezo yaliyotolewa katika mapitio ya utekelezaji ya Wizara kwa mwaka 2019/2020; Mpango Mkakati wa Nne wa Wizara; Mikakati ya Kitaifa na Kimataifa, Dira ya Maendeleo 2050, Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020/2025 na maagizo ya Serikali; vipaumbele hivyo vinagusa maeneo yafuatayo:-

- i. Kuimarisha huduma za afya ya mama na mtoto ili kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi;
- ii. Kuimarisha uwezo na utayari wa kupambana na maradhi ya mripuko na majanga ya kiafya;
- iii. Kuongeza nguvu katika usimamizi wa miradi ya maendeleo;

- iv. Kusimamia utekelezaji wa sheria na taratibu zilizowekwa zikiwemo za manunuzi;
- v. Kuendelea na jitihada za kutokomeza ugonjwa wa Malaria Zanzibar;
- vi. Kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa vyta utibabu na uchunguzi;
- vii. Kuweka mfumo endelevu wa kugharamia huduma za afya;
- viii. Kuendelea na hatua za kuanzisha bima ya afya;
- ix. Kuimarisha nguvu kazi, kusimamia utendaji pamoja na kuandaa mazingira mazuri ya kazi;
- x. Kuimarisha mapambano dhidi ya vitendo vyta ukatili kwa wanawake na watoto;
- xi. Kuimarisha hifadhi ya jamii kwa wanaoishi katika mazingira magumu; na
- xii. Kuendeleza mapambano dhidi ya maradhi ya kuambukiza na yasiyoambukiza

SHUGHULI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

118. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha vipaumbele vilivyoainishwa hapo juu vinafikiwa, Wizara itatekeleza shughuli zilizopangwa kuitia programu husika kama ifuatavyo:-

PROGRAMU YA KINGA NA ELIMU YA AFYA (PH0301)

119. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara imetenga shilingi **34,570,812,000** sawa na asilimia **17.5** ya bajeti ya Wizara kwa ajili kutekeleza shughuli zilizopangwa na programu hii ambazo zinahusisha:-

- i. Kuimarisha mifumo ya miundombinu ya kiafya ya kujiweka tayari katika kudhibiti (preparedness and response) athari zitokanazo na majanga ya kiafya na maradhi ya miripuko;
- ii. Kuendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Afya ya Jamii ili kuimarisha kinga dhidi ya maradhi ya kuambukiza;
- iii. Kutekeleza Mkakati wa kutokomeza Kipindupindu Zanzibar (ZACCEP 2018/27) sambamba na kutoa chanjo ya Kipindupindu katika Shehia 33 zinazopata miripuko ya mara kwa mara;
- iv. Kuendelea kuimarisha huduma za matibabu ya ugonjwa wa UKIMWI kwa kuongeza kiwango cha kufubaza cha chini ya kopi 1,000 za virusi vya ukimwi kwa zaidi ya asilimia 95 pamoja na kuongeza upatikanaji wa huduma za kuzuia maambukizo ya virusi vya UKIMWI kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto;

- v. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za Homa ya Ini B pamoja na kutoa chanjo ya homa ya Ini katika jamii kwa makundi yaliyo hatarishi katika kupata maradhi haya; na kuongeza kiwango cha uibuaji wa wagonjwa wa Kifua Kikuu na Ukoma katika jamii hasa katika maeneo yanayoshukiwa kuwa na wagonjwa wengi zaidi
- vi. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya ya uzazi na afya ya mama na mtoto katika ngazi ya msingi sambamba na kuongeza vituo vya daraja la pili kwa kutoa huduma za kujifungua;
- vii. Kuendelea na jitihada za kumaliza maradhi ya kichocho, na vikope kupitia tafiti, uchunguzi, na kampeni maalum za jamii hasa katika maeneo yenye viwango vikubwa zaidi vya maambukizi;
- viii. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za msingi za macho katika vituo vya afya vya msingi (PHCUs na PHCU+) sambamba na kuanzisha huduma maalum za uchunguzi wa macho kwa watoto skulini; na
- ix. Kutekeleza Mwongozo Shirikishi wa Mfumo wa Ufutiliaji wa Magonjwa Toleo namba tatu (3) la Shirika la Afya Ulimwenguni kanda ya Afrika na kuhakikisha taarifa za maradhi katika vituo na hospitali zikiwemo taarifa katika ngazi ya jamii (Community IDSR) zinaunganishwa katika mfumo wa kielektroni (e-IDSR)

PROGRAMU YA TIBA (PH0302)

120. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, programu hii imepangiwa kutumia shilingi **122,705,936,000** sawa na asilimia **62.0** kwa ajili ya kutekeleza shughuli kuu zinazotekelizwa na programu hii. Hivyo, naliomba Baraza hili liidhinishe shughuli hizo ambazo ni:-

- i. Kutoa huduma za uchunguzi na matibabu katika hospitali za Serikali;
- ii. Kuimarisha miundombinu ya hospitali ikiwemo ukarabati wa Hospitali za vijiji, Wilaya na Mkoa; na ujenzi wa nyumba za wafanyakazi;
- iii. Kuimarisha upatikanaji wa dawa na vifaa vya utibabu kwenye ngazi zote za huduma;
- iv. Kuziimarisha huduma za mkono kwa mkono katika hospitali;
- v. Kuongeza uelewa wa jamii juu ya matumizi ya matokeo ya uchunguzi wa vinasaba (DNA) katika kupambana na kesi za udhalilishaji;
- vi. Kuendelea kushikilia ithibati na hati ya viwango vya ubora kimataifa; na
- vii. Kukamilisha ujenzi wa maabara ya kisasa ya Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi.

**PROGRAMU HIFADHI YA JAMII, MAENDELEO YA JINSIA NA WATOTO
(PH0303)**

- 121. Mheshimiwa Spika**, jumla ya shilingi **15,005,305,000** sawa na asilimia **7.6** ya bajeti zimepangwa kutumika kwa shughuli mbali mbali zinazoratibiwa na programu hii zitakazotekelawa kupitia programu ndogo ya huduma za jinsia na watoto na programu ndogo ya huduma za uhifadhi wa jamii ambazo ni pamoja na:-
- i. Kufanya ukarabati mkubwa katika makao ya wazee Welezo na Sebleni;
 - ii. Kusimamia uendeshaji wa mpango wa malipo ya pensheni jamii;
 - iii. Kukamilisha ujenzi wa uzio katika makao ya wazee ya Welezo;
 - iv. Kutayarisha mkakati wa mawasiliano ili kuimarisha mifumo ya familia na kupambana na vitendo vya ukatili kwa watoto;
 - v. Kujenga uwezo na ushiriki wa watoto katika mabaraza ya watoto; na
 - vi. Kuendeleza usawa wa kijinsia na kuwawezesha wanawake kiuchumi.

PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA (PH0305)

122. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022, wizara imepanga kutumia shilingi **25,586,447,000** sawa na asilimia **12.9** ya bajeti kwa ajili ya shughuli zilizomo katika programu hii. Shughuli ambazo zitatekelezwa ni pamoja na:-

- i. Kuendelea kusomesha wataalamu bingwa wa kada za afya ili kupunguza uhaba uliopo;
- ii. Kutekeleza Mkakati wa Kidijitali wa Afya na Mkakati wa Taarifa za Afya;
- iii. Kufanya mapitio ya Sera na sheria zinazohitaji kufanyiwa marekebisho;
- iv. Kuratibu shughuli za miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa nyumba za madaktari katika Hospitali ya Abdulla Mzee, ukarabati wa Hospitali ya Wete na Hospitali Mnazi Mmoja;
- v. Kufanya utafiti wa matumizi ya fedha za afya (Public Expenditure Review);
- vi. Kuendelea na shughuli za kufanya tafiti za maradhi ya kuambukiza na yasioyoambukiza; na
- vii. Kuendelea na utafiti wa “Sero Prevalence Study” kwa magonjwa ya mripuko ikiwemo Korona.

PROGRAMU YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA (H02)

123. Mheshimiwa Spika, jumla ya shilingi **20,371,200,000** zimepangwa kutumika kwa shughuli mbali zinazoratibiwa na Hospitali ya Mnazi Mmoja zikiwemo:-

- i. Kufanya ukarabati mkubwa na upanuzi wa hospitali ya Mnazi Mmoja kupitia mradi wa BADEA, “Saudi Fund” na “Kuwait Fund” kwa kufanya shughuli mbali mbali zikiwemo:-
 - a. Ujenzi wa jengo la kisasa la kutolea huduma za upasuaji wa moyo na mifupa,
 - b. Ununuzi wa mashine za kisasa za uchunguzi pamoja na samani za hospitali,
 - c. Kujenga jengo la kisasa kwa ajili ya huduma za haraka na wagonjwa wanaolipia huduma,
- ii. Kufanya matengenezo (service) ya mashine za uchunguzi na utibabu; na
- iii. Kugharamia mafunzo ya utumishi wa umma kwa wafanyakazi **600** ambao hawajathibitishwa.

SHUKRANI

124. Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba dhana nzima ya utoaji wa huduma bora za afya, kulinda ustawi wa jamii pamoja na kupambana na vitendo vyote vya udhalilishaji vya wanawake na watoto linahitaji nguvu za pamoja baina ya serikali, taasisi binafsi na jamii. Kwa mantiki hiyo, mafanikio yaliyofikiwa yalitokana na kuwepo mashirikiano mazuri na taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali, Mashirika ya Kimataifa, sekta binafsi na mtu mmoja mmoja. Wizara inatambua na kuthamini michango yao ya kifedha na kiutaalamu waliyoipatia katika kufanikisha malengo ya Wizara. Hivyo basi, kwa niaba ya wizara natoa shukrani za dhati kwa wote walioshirikiana nasi katika utekelezaji wa mwaka 2020/2021. Aidha, nawashukuru Wajumbe wote wa Baraza hili pamoja na wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika, kwa hakika mmekuwa mstari wa mbele katika kutoa michango na ushauri. Nawaomba tuendelee kushirikiana ili tuilinde jamii ya Wazanzibari.

125. Mheshimiwa Spika, nichukuwe fursa hii kuwashukuru watendaji wa Wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu Dr. Omar Dadi Shajak, Naibu Katibu, Mkurugenzi Mkuu pamoja na wakurugenzi wote kwa msaada mkubwa wanaonipatia na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya uwaziri kwa unafuu. Aidha, mashirikiano yao ndiyo yaliyonifanya mimi leo hii kuisoma hotuba hii mbele ya wajumbe wa Baraza hili.

- 126. Mheshimiwa Spika**, mafanikio yaliyopatikana yalitokana na msukumo mkubwa kutoka kwa Serikali za nchi marafiki, taasisi, mashirika ya kitaifa na kimataifa. Mimi binafsi na wafanyakazi wote pamoja na wananchi kwa ujumla tunatoa shukurani za dhati kwao. Ndugu zetu hawa wamekuwa na mchangano mkubwa katika kutusaidia kutoa huduma kwa ufanisi na kwa wepesi. Nawaomba wote waendelee kuwa nasi bila kusita au kuchoka. Shukurani ziende kwa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, Serikali ya Cuba, Serikali ya Watu wa Marekani, Spain, Norway, India, Dernmark, UAE, Jumuiya ya Afrika Mashariki, Saudia, Kuwait, Misri na nyenginezo. Pia shukurani hizi ziende kwa Wizara zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana nasi katika kuhakikisha malengo ya wizara yanafikiwa.
- 127. Mheshimiwa Spika**, nitoe shukurani kwa mashirika ya kimataifa na kikanda yakiwemo WHO, UNICEF, UNFPA, UNDP, UN Women, ILO, Help Age International, Milele Foundation, Costech PEPFAR, PMI, GFATM, Water AID, Rotary UK, PATH, USAID, AMREF, Save the Children, IOM, Sight Savers International, Hauckland University Hospital, CDC na wale wote ambao sikuwaorodhesha.

HITIMISHO

MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

- 128. Mheshimiwa Spika**, nawaomba wajumbe wa kamati waipokee taarifa hii ya mapendekeo ya bajeti, waijadili, waichangie kwa uwazi na hatimae wakubali mapendekezo ya matumizi ya shilingi **197,868,500,000** kwa Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto (Fungu H03). Kati ya hizo shilingi **36,577,900,000** kwa ajili ya mishahara, shilingi **51,809,508,000** kwa matumizi uendeshaji wa ofisi; shilingi **4,385,000,000** kwa taasisi zinazopokea ruzuku na shilingi **105,096,092,000** kwa kazi za maendeleo. Aidha, waidhinishe mapendekezo ya shilingi **20,371,200,000** kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja (Fungu H02). Kati ya hizo shilingi **14,808,900,000** kwa ajili ya mishahara na shilingi **5,562,300,000** kwa matumizi ya shughuli za uendeshaji (**Kimbatisho namba 7**).
- 129. Mheshimiwa Spika**, naomba pia Baraza hili liridhie makusanyo ya shilingi **5,038,053,000** kwa Fungu la Wizara (H03) na **shilingi 1,379,800,000** zikusanywe na Hospitali ya Mnazi Mmoja (H02) kutoka katika vyanzo vya ukusanyaji wa mapato vya kwa ajili ya kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali.
- 130. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja

NASSOR AHMED MAZRUI (MBM)

**WAZIRI WA AFYA, USTAWI WA JAMII, WAZEE, JINSIA NA WATOTO
ZANZIBAR.**

Kiambatisho Namba 1: Muhtasari wa Matumizi kwa Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto (Julai, 2020 - Machi, 2021)

Fungu H03: Wizara ya Afya H02: Hospitali ya Mnazi Mimoja	Makadirio ya Fedha 2020/2021	Makadirio ya Fedha (Julai, 2020 - Machi, 2021)	Fedha Zilizopatikana (Julai, 2020 - Machi, 2021)	Asilimia ya Fedha Zilizopatikana (Julai, 2020 - Machi, 2021)	Asilimia ya Fedha zilizopatikana kwa mwaka 2020/2021
Mshahara					
Unguja	10,725,507,000	8,044,130,250	9,303,350,992	115.7	86.7
Pemba	8,625,993,000	6,469,494,750	7,327,213,695	113.3	84.9
Jumla ndogo	19,351,500,000	14,513,625,000	16,630,564,687	114.6	85.9
Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi					
Unguja	33,779,479,650	30,061,651,163	15,141,852,493	50.4	44.8
Pemba	1,533,620,350	1,115,794,034	267,698,338	24	17.5
Jumla Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi	35,313,100,000	31,177,445,197	15,409,550,831	49.4	43.6
JUMLA MATUMIZI YA KAWAIDA	54,664,600,000	45,691,070,197	32,040,115,518	70.1	58.6
Ruzuku	2,924,400,000	2,193,300,001	1,550,346,464	70.7	53
Jumla Ruzuku	2,924,400,000	2,193,300,001	1,550,346,464	70.7	53
Fedha za Maendeleo					
SMZ	20,996,000,000	17,201,451,985	2,831,058,366	16.5	13.5
Wahisani	21,651,100,000	19,851,209,787	2,735,702,541	13.8	12.6
JUMLA MAENDELEO	42,647,100,000	37,052,661,772	5,566,760,907	15	13.1
JUMLA FUNGU (H03)	100,236,100,000	84,937,031,970	39,157,222,889	46.1	39.1
Fungu H02: Hospitali ya Mnazi Mimoja					
Mishahara	12,249,400,000	9,187,049,997	10,057,978,258	109.5	82.1
Matumizi ya Uendeshaji wa Hospitali	5,099,200,000	4,633,532,922	2,581,051,896	55.7	50.6
JUMLA FUNGU (H02)	17,348,600,000	13,820,582,919	12,639,030,154	91.5	72.9
JUMLA KUU (H03 & H02)	117,584,700,000	98,757,614,889	51,796,253,043	52.4	44.1
Ustawi wa Jamii, Mnendeleo ya Jinsia na Watoto					
Ustawi wa Jamii na Wazee	10,544,035,080	7,908,026,310	6,236,774,070	78.9	59.1
Jinsia na Watoto	1,009,759,016	757,319,262	176,056,685	23.2	17.4
JUMLA YA PROGRAMU	11,553,794,096	8,665,345,572	6,412,830,755	74	55.5

Kiambatisho Namba 2: Taarifa ya Makusanyo ya Wizara ya Afya Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto; Julai, 2020 - Machi, 2021; na Makadirio ya Makusanyo kwa mwaka 2021/2022

Kifungu	GFS code	Maelezo	Makusanyo Hali 2019/2020	Makadirio ya Makusanyo 2020/2021	Fedha Zilizokusanywa (Julai,2020 - Machi,2021)	Asilimia ya Makusanyo (Juli,2020 - Machi,2021)	Makadirio ya Makusanyo April Juni, 2021	Makadirio ya Makusanyo 2021/2022
H0301	Programu ya Kinga na Elimu ya Afya							
	142200	Administraton Fees						
	1422035	Shuhuda ya mraadhi	99,399,000	148,251,000	1,512,693,686	>100	44,645,938	2,300,720,000
	1422050	Ada ya uchunguzi wa vyombo vya usafiri na abiria	43,697,030	66,305,000	17,093,400	25.7	13,665,375	80,650,000
	1422051	Uchunguzi wa afya ya wafunyalizi	45,200,248	79,000,000	33,262,500	42.1	19,273,500	80,603,000
	Jumla ndogo		188,196,278	293,756,000	1,563,849,586	>100	77,584,813	2,461,973,000
H0302	Programu ya Tiba							
	1422095	Ada ya kibaki cha tiba asili	21,771,296	36,240,000	64,724,432	>100	9,610,000	93,952,000
H0313	1422118	Usajili na leseni kwa Wasanzu						116,210,000
H0314	1422118	Usajili na leseni kwa Madaktari						130,000,000
H0315	1422118	Usajili na leseni kwa wanawake Afya ya Mazingira						182,001,000
H0316	1422118	Usajili na leseni kwa Huduma za Hospitali Binabti						250,963,000
	Jumla ndogo		21,771,296	36,240,000	64,724,432	>100	9,610,000	773,126,000
H0303	Programu ya Hisafishi ya Jamii Maendeleo ya Jinsia na Watoto							
	1422078	Ustawi wa Jamii						900,100,000
	Jumla ndogo						900,100,000	
H0305	Programu ya Uratibu wa Sera za Afya na Utawala							
	1422084	Invaraka za Zabuni	7,200,000	18,000,000	6,263,000	34.8	3,100,000	70,000,000
	1422094	Taasisi ya Utatifu wa Afya						105,904,000
	1422051	Huduma za uchunguzi wa afya Pemba						726,904,000
	Jumla ndogo		7,200,000	18,000,000	6,263,000	34.8	3,100,000	902,854,000
JUMLA KUU FUNGU H03:			217,167,574	347,996,000	1,634,837,818	>100	90,294,813	5,038,053,000
Fungo - H02								
H0201	Huduma za Uongozi na Utawala							
	1422073	Malipo ya huduma za afya kwa wagonjwa wa Bima	220,667,000					243,915,000
	1422078	Ukodishaji wa mseneo ya Kibasharn						7,440,000
	1423003	Kitengen cha huduma za haraka	473,641,000					
H0202	Huduma za Uchunguzi na matibabu							
	1422094	Mapato ya utatifu		200,000,000	30,995,000		52,000,000	
	1423003	Kitengen cha huduma za haraka		475,000,000	549,798,374	>100	132,100,000	1,327,548,000
	Jumla H02		629,879,316	675,000,000	580,793,374	86	49,685,942	1,379,821,000
JUMLA KUU WIZARA YA AFYA UJWJW			847,046,890	1,022,996,000	2,214,830,392	>100	139,388,755	6,417,874,000

**Kiambatisho Namba 3a: Thamani ya Dawa zilizopokelewa
kutoka Washirika wa Maendeleo
Julai, 2020 - Machi, 2021**

No.	KUTOKA	THAMANI (TSH)
1	GLOBAL FUNDS	3,763,007,697
2	UNFPA	1,106,948,460
3	DANIDA	793,251,710
4	CHINA	97,474,360
5	UNICEF	1,122,769,564
6	INDIA	295,213,840
7	WHO	1,290,041,750
8	IFAKARA	7,500,000
JUMLA KUU		8,476,207,381

**Kiambatisho Namba 3b: Mchanganuo wa Makisio ya Ununuzi
wa Dawa na vifaa tiba kwa mahitaji
ya Mwaka 2021/2022**

Aina ya dawa naVifaa tiba	Makisio Tsh.
Dawa muhimu (Essential Medicines and Medical supplies)	25,174,065,278
Vitendanishi vya Maabara (Laboratory Reagents and Consumables)	5,875,335,527
Vifaa vya Uchunguzi wa Mionzi (Imaging and Radiology commodities)	2,830,905,101
Vifaa Tiba (Standard Medical Equipment)	12,083,036,522
Dawa za Saratani (Oncology unit)	2,521,356,342
Huduma za Figo (Dialysis Services)	1,854,492,000
Vifaa kwa ajili ya Huduma za Korona	3,122,434,881
Huduma za Damu Salama (Blood Transfusion Services)	758,248,646
Huduma za Matibabu ya Macho	842,356,654
Huduma za Matibabu ya Mifupa (Orthopedic surgery)	465,211,000
Huduma za Matibabu ya Meno (Dental materials)	140,627,951
Dawa na Vifaa vya uchunguzi wa Malaria	124,999,000
Matibabu ya Viungo (Physiotherapy)	128,863,070
Vifaa vya matengenezo ya Viungo Bandia (Orthopedic workshop)	64,860,512
Huduma za Matibabu ya Sikio, Pua na Koo (ENT)	3,395,951,378
Dawa na Vifaa vya uchunguzi wa Homa ya Ini (Hepatitis)	687,962,237
Huduma za Upasuaji wa Kichwa na uti wa mgongo (Neurosurgery)	86,377,568
Jumla Kuu (Tsh)	60,157,083,667

**Kiambatisho Namba 4: Wafanyakazi wapya walioajiriwa
katika kipindi cha Julai 2020 - Machi
2021 ya Mwaka 2021/2022**

Kada	Unguja	Pemba	Jumla
Afisa Ushauri Nasaha	38	4	42
Daktari	20	6	26
Afisa Afya Mazingira	119	46	165
Afisa Kumbukumbu	6	-	6
Afisa Lishe	2	1	3
Afisa Maabara	5	-	5
Afisa Tehama	3	-	3
Dereva	4	-	4
Mlinzi	31	3	34
Wahudumu	449	76	525
Muuguzi	73	71	144
Fundi Sanifu Dawa	11	2	13
Mkemia	1	1	2
Mzoeza Viungo	5	-	5
Mfamasia	7	2	9
Microbiologist	3	1	4
Fundi Sanifu Vifaa Tiba	1	-	1
Afisa Uchumi	1	-	1
Afisa Ustawi wa Jamii	40	-	40
Afisa Mfumo wa Taarifa za Afya	1	-	1
Mhandisi Majengo	1	-	1
Karani Masjala	3	-	3
Afisa Uhusiano	1	-	1
Tabibu Meno	-	2	2
Afisa Ufuutiliaji	1	1	2
Afisa Sheria	2	-	2
Special Gang	1	-	1
Katibu Muhtasi	1	-	1
Food Inspector	-	1	1
Assistance Biologist	1	-	1
Afisa Manunuzi	3	-	3
Afisa Tabibu	19	3	22
Jumla	853	220	1,073

**Kiambatisho Namba 5(a): Idadi ya Wafanyakazi waliorudi masomoni,
Julai 2020 hadi Machi 2021**

No.	Fani	Diploma	Shahada	Uzamili	Daktari Bingwa	Uzamivu	Jumla
1	Allied Science	-	3	2	-	-	5
2	Laboratory	-	-	3	-	-	3
3	Internal Medicine	-	15	1	5	-	21
4	Nursing	-	14	7	-	-	21
5	Pharmacy	1	5	-	-	-	6
6	Non Medical	3	2	5		1	11
JUMLA		4	39	18	5	1	67

Kiambatisho Namba 5(b): Ildadi ya wafanyakazi walioperekwa Masomoni Julai 2020 hadi Machi 2021 na fani wanazochukuwa

No.	Fani	Diploma	Diploma ya juu	Shahada	Uzamili	Daktari Bingwa	Uzamivu	Jumla
1	Allied Science	-	-	9	7	-	1	17
2	Anaesthesia	-	-	1	-	1	-	2
3	Biomedical Engineering	-	-	2	-	-	-	2
4	Clinical Officer	-	4	-	-	-	-	4
5	Diagnostic	-	-	1	-	-	-	1
6	Laboratory	-	-	9	2	-	-	11
7	Medical Imaging	-	-	2	-	1	-	3
8	Internal Medicine	-	-	2	-	46	1	49
9	Nursing	-	-	12	2	-	2	16
10	Pharmacist	-	-	20	7	-	-	27
11	Non-Medical	3	-	4	11	-	1	19
Jumla		3	4	62	29	48	5	151

Kiambatisho Namba 6: Orodha ya Mapendekezo ya Tafiti zilizopokelewa na kuitishwa kuanzia Julai, 2020 hadi Machi, 2021

N.º	Jina la Pendekazo (Proposal)
1	Trachoma impact survey in Micheweni, Zanzibar
2	Maximising benefit and minimising the harm of covid-19 control measures on child and women's health in Tanzania, Zimbabwe, Uganda and Ghana
3	Personalized and improved perinatal health in Zanzibar through machine-learning supported decision support
4	Evaluation of antibody and antigen rapid diagnostic test (RTD) for COVID19 in the EAC partner State.
5	Determining the prevalence and intensity of schistosomiasis and soil transmitted helminthes to inform the national strategy (Pilot)
6	Assessing quality of counselling and satisfied with services among family planning clients in selected health facilities in main land Tanzania and Zanzibar: Across sectional survey
7	End term evaluation of community-based mental health services project
8	Sero-Epidemiological investigation of Covid-19 infection in Zanzibar-Tanzania.
9	Understanding community and healthcare workers knowledge, perceptions, practices and capacity of health facilities to diagnose Female Genital Schistosomiasis in Zanzibar (Unguja and Pemba), Tanzania.
10	Performance of Maternal and Perinatal Death Surveillance and response MPDSR in Zanzibar for the Period of January to December 2019
11	Formative research on the value of neonatal life in Mbeya and Kaskazini Pemba Region, Tanzania.
12	Final Evaluation of Health Information System Project in Tanzania Mainland and Zanzibar, Tanzania.
13	Harnessing PPNDC infrastructure to assess impact on MNCH during COVID-19 pandemic.
14	Cross-sectional survey on soil transmitted helminth infection in schoolchildren in Pemba.
15	Efficacy and safety of Moxidectin and Albendazole compared to ivermectin and albendazole co-administration in adolescents infected with Trichuris trichuria Pemba, Zanzibar: a randomized controlled trial.
16	Compliance with public health and social measures to interrupt the Transmission of COVID-19 in Zanzibar by Zanzibar Health Research Institute, Zanzibar Ministry of Health, World Health Organization.
17	Comparative genomics of adult necatoramericanus worms exposed to different levels of ALB: new insights into the mechanisms of anthelmintic resistance.

Kiambatisho Namba 7: Mchanganuo wa Maombi ya Fedha kwa mwaka 2021/2022

Maelezo ya Matumizi Wizara ya Afya Ustawi wa Jamii Wazee Jinsia na Watoto	Mehango wa Serikali	Matumizi ya Shughuli za Maendeleo Msaada Washirika wa Maendeleo	Jumla Fedha za Maendeleo	Matumizi ya Kawaida	Jumla Kuu
Programu ya Kinga na Elimu ya Afya – P10301					
Huduma za Kinga na Elimu ya Afya	-	-	-	20,154,666,000	20,154,666,000
Mradi Shirikishi wa Hudurra za Afya ya Mama na Mto	1,000,000,000	2,630,199,000	3,630,199,000	-	3,630,199,000
Mradi Shirikishi wa UKIMWI, Honza ya Ini, Kisii Kikuu na Ukomaa	1,000,000,000	6,221,572,000	7,221,572,000	-	7,221,572,000
Mradi wa Kamaliza Malaria Zanzibar	713,545,000	2,850,830,000	3,564,375,000	-	3,564,375,000
Jumla Ndogo	2,713,545,000	11,702,601,000	14,416,146,000	20,154,666,000	34,570,812,000
Programu ya Tiba - P10302					
Programu ndogo ya uchunguzi	-	-	-	3,731,026,000	3,731,026,000
Programu ndogo ya matibabu	-	-	-	33,694,964,000	33,694,964,000
Mradi wa Kupandisha Hadhi Hospitali za Wilaya na Vijiji	8,000,000,000	-	8,000,000,000	-	8,000,000,000
Mradi wa Kupandisha Hadhi hospitali ya Mtaazi Mmeja	10,279,946,000	-	10,279,946,000	-	10,279,946,000
Kuimariisha Hudume za Densu Salama	55,000,000,000	55,000,000,000	55,000,000,000	-	55,000,000,000
Mradi wa Upanzu wa Hospitali ya Wete	100,000,000	6,900,000,000	7,000,000,000	-	7,000,000,000
Mradi wa Ujenzi wa Bohari Kuu ya Dawa Pemba	3,000,000,000	-	3,000,000,000	-	3,000,000,000
Ujenzi wa Maabaraza Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodoozi	2,000,000,000	-	2,000,000,000	-	2,000,000,000
Jumla Ndogo	78,379,946,000	6,900,000,000	85,279,946,000	37,425,990,000	122,705,936,000

Kiambatisho Namba 7: Mchanganuo wa Maombi ya Fedha kwa mwaka 2021/2022

Maelezo ya Matumizi Wizara ya Afya Ustawi wa Jamii Wazee Jinsia na Watoto	Mehango wa Serikali	Matumizi ya Shughuli za Maendeleo Msadaa Washirika wa Maendeleo	Jumla Fedha za Maendeleo	Matumizi ya Kawaida	Jumla Kuu
Programu ya Hifadhi ya Jamii, Maendeleo ya Jamii, Maendeleo ya Watoto - PH0304					
Programu ndogo ya Hifadhi ya Jamii	-	-	-	10,267,267,000	10,267,267,000
Programu ndogo ya Jinsia na Watoto	-	-	-	838,038,000	838,038,000
Mradi wa Hifadhi ya Wazee	3,900,000,000	-	3,900,000,000	-	3,900,000,000
Jumla Ndogo	3,900,000,000	-	3,900,000,000	11,105,305,000	15,005,305,000
Programu ya Uendeshajii na Utaribu wa Wizara - PH0305					
Programu ndogo ya Utaribu na Uendeshajii	-	-	-	8,335,051,000	8,335,051,000
Programu ndogo ya Mpango, Sera na Utarifi	-	-	2,238,164,000	-	2,238,164,000
Programu ndogo ya Utaribu wa Shughuli za Afya Penha	-	-	-	13,513,232,000	13,513,232,000
Mradi wa Kuimariishi Taasisi ya Utarifi wa Afya	1,500,000,000	-	1,500,000,000	-	1,500,000,000
Jumla Ndogo	1,500,000,000	-	1,500,000,000	24,086,447,000	25,586,447,000
JUMLA FUNGU H03	86,493,491,000	18,602,601,000	105,096,092,000	92,772,408,000	197,868,500,000
Hospitali ya Mnazi Mmoja (Fungu H02)					
Programu ya Uchunguzi na Matibabu	-	-	-	813,382,000	813,382,000
Programu ya Uendeshajii na Utaribu wa Hospitali ya Mnazi Mmoja	-	-	-	19,557,818,000	19,557,818,000
JUMLA FUNGU H02	-	-	-	20,371,200,000	20,371,200,000
JUMLA KUU H03 NA H02	86,493,491,000	18,602,601,000	105,096,092,000	113,143,608,000	218,239,700,000